

SAUTIZETU

A photograph of a man sitting on a stone ledge next to a public toilet. The man is wearing a light-colored polo shirt and blue jeans. He is looking down at something in his hands. The toilet is a simple, white, pedestal-style toilet with a red flush pipe. The background is a wall made of corrugated metal, painted in shades of blue and green. The floor is made of irregular, reddish-brown stones. The overall scene suggests a rural or semi-rural environment with basic sanitation facilities.

kujumuishwa

THE OPEN SOCIETY INITIATIVE
FOR EASTERN AFRICA

kuheshimu
haki za
binadamu

SAUTIZETU

THE OPEN SOCIETY INITIATIVE FOR EASTERN AFRICA

**MKURUGENZI MTENDAJI
BINAIFER NOWROJEE**

**WAHARIRI
EMMA DAY
UMRA OMAR**

**MHARIRI MSAIDIZI
GLADYS ONYANGO**



**MKURUGENZI UBUNIFU
ASSEGID GESSESSE**

**WAKURUGENZI SANAA
NAZRAWI GHEBRESELASIE
CHRIS COGSWELL**

OSIEA inakuza ushiriki wa wananchi katika utawala wa kidemokrasia, utawala wa sheria, na kuheshimu haki za binadamu na kutoa misaada, kuanzisha programu na kuwaleta pamoja viongozi mbalimbali wa vikundi na asasi za kiraia.

OSIEA inajukumu kubwa la kuhamasisha kuwepo kwa uwazi na mijadala makini kuhusu masuala muhimu ya wananchi wa eneo la Afrika Mashariki

OSIEA inasaidia jitihada hizo nchini Kenya, Tanzania, Uganda, Sudan pamoja na kwa mashirika ya kikanda yanayofanya kazi eneo lote la Afrika Mashariki

Ofisi ya Nairobi: ACS Plaza, Barabara ya Lenana, S.L.P 2193-00202, Nairobi, Kenya

Hili ni toleo la tatu la Jarida la Sauti Zetu linalotolewa kila mwaka na shirika la Open Society Initiative for East Africa (OSIEA). Shirika la OSIEA huandaa jarida hili kwa malengo ya kutoa fursa ya ushiriki wa wazi na makini kwa wananchi katika masuala muhimu kwa jamii ya kuendeleza maadili ya uwazi nchi za Afrika Mashariki.



Tabariri

Msingi muhimu wa kujenga jamii yenye uwazi ni kuwepo kwa usawa, umoja kwa watu wa aina zote na kujumuishwa. Toleo hili la Sauti Zetu linabainisha maana na mwelekeo wa dhana hizi, na vikwazo kwenye kufanikisha uwepo wa dhana hizi katika eneo la Afrika Mashariki.

Tunaishi katika jamii zenye watu wa aina nyingi waliokulia mazingira na historia tofauti, imani tofauti na mifumo tofauti ya maisha. Lakini tofauti hizi si kitu kinachotugawa. Kinachotugawa ni kutokuwa tayari kwetu kuzipokea na kuziishi tofauti hizi.

Kwa kukosa uvumilivu, tunawatenga na kuwanyanyapaa baadhi ya watu ndani ya jamii zetu. Tunajiweka mbali nao wenzentu waliotofauti – wale wasiofanana, wasiotenda, au wasioonekana kuwa kama “sisi”. Tunawaona na kuwahukumu watu au jamii fulani kama ni “viumbe duni,” na hivyo, hawastahili kutendawa sawa na wengine. Tunadhoofisha uwezo wao kushiriki kikamilifu kwenye maisha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Tunawafanya wasionekane na kuwanyima nguvu za kufanya maamuzi kwenye masuala yanayohusu maisha yao. Kibaya zaidi, tunawaona kama vitisho kwetu na hivyo kuwafanyiwa ukatili mbaa na ukiukaji mkubwa wa haki zengine.”

Na msingi wa ubaguzi na kutengwa unahusishwa na jinsia ya mtu, kabila, dini, utaifa, uathirika wa Virusi vya Ukimwi (VVU) . Pia inaweza kufanywa kwa watu wenye ulemavu, makundi ya watu wachache yanayoamini mahusiano ya mapenzi ya jinsia moja, au wafugaji. Mtu yeyote anayeonekana kuwa tofauti na hali iliyozoeleka ndani ya jamii pana anaweza kuwa mlengwa wa hila na vitendo vya wazi vya ubaguzi na kudunishwa ambavyo vinazuia kupata fursa, haki na rasilimali kwa msingi sawa na wengine. Mara nyingi wito wa kutaka kutukuza kabila, utamaduni au dini za makundi makubwa hutumika kama mwamvuli wa kuwabinyia watu haki zao za binadamu.

Licha ya kuwepo kwa Azimio la Haki za Watu wenye Ulemavu ambalo limeridhiwa na nchi zote za Afrika Mashariki, hali iliyozoeleka eneo zima la Afrika Mashariki ni kubaguliwa kwa watu wenye ulemavu wa mwili na akili. Ingawa idadi ya wanawake ni nusu ya jamii yote, wanawake na wasichana bado wako kwenye hatari kubwa ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wakiwa nyumbani na nje ya nyumbani, na bado wanaendelea kupigania haki na fursa sawa. Kundi lililotengwa kwa utaratibu katika eneo lote la Afrika Mashariki ni wafugaji, ambao maisha yao ya ufugaji wa ng'ombe wa kuhamahama, yanaleta changamoto kwenye sera za sasa za umiliki wa ardhi. Makundi ya watu wachache wenye kufuata mahusiano ya kimapenzi tofauti na jamii kubwa kama vile mashoga mara nyingi wanasubuliwa kupitia kauli za chuki, kuteswa na kufanyiwa vurugu na ukatili. Kupigania uraia ni jambo linaloonekana sana katika Ukanda wa Afrika Mashariki ambako sera za uraia mara nyingi huwabagua baadhi ya watu kwa misingi ya kabila au jinsia.

Lakini kwa sasa kuna nguvu ya kukabiliana na nguvu hizo eneo lote la Afrika mashariki. Jamii zilizotengwa zinarejesha uwezo wao na kufanyakazi ya kuondoa vikwazo vya kisheria na kimitazamo ambavyo vinazuia ushiriki wao kama raia wenye haki sawa ndani ya jamii. Wanajihusisha na utetezi/uchechemuzi, kurekebisha sheria, madai kimkakati na miradi ya elimu kwa jamii pana kupambana na ubaguzi, chuki na vitendo viovu

Sauti zilizomo katika toleo hili zimegusa baadhi ya harakati za kuhakikisha makundi haya yanatambuliwa kisheria, yanapata haki, uhuru na usalama wa kwa kila mtu, na kuwa huru dhidi mateso, vitendo vya ukatili na heshima ya faragha kwa kila mtu. Katika ofisi yetu ya Open Society Initiative for Eastern Africa, tunaunga mkono kuheshimu asili ya mtu, utofauti miongoni mwa watu na ubinadamu wa watu wote.

Kwetu sisi, binadamu wote ni sawa

Binaifer Nowrojee
Mkurugenzi Mtendaji

katika toleo hili



Kuwafuja Vijana Wetu



Kukatakata Mapanga Vijana Wetu



Bado Tunasongea Mbele



Wafugaji wa Kikarimojong



Wanawake nchini Uganda



Kufungiwa Ndani



Watu Wafupi wafupi



Jitihada za Kutafuta Uraia Sudan Kusini



Wanawake Wanasheria Zanzibar



Haki za Wafugaji nchini Tanzania



Wananchi Daraja la Pili



UKOSEFU WA AJIRA KWA VIJANA WA KENYA

KUWAFUJA VIJANA WETU

NA JAKI MBOGO

IDADI YA VIJANA NCHINI KENYA INAFIKIA MILIONI 9.1 (NI KIASI CHA 32% YA WATU WOTE), WAKIWA KARIBU 60% YA JUMLA YA NGUVU KAZI YA TAIFA

DANIEL ONYANGO alizaliwa na kukulia Korogocho, mtaa duni wa nne kwa ufukara nchini Kenya. Kwa sasa amejiunga na masomo ya shahada katika Chuo Kikuu cha Nairobi pia ni mwanzilishi wa shirika linalojishughulisha na masuala ya sanaa za jamii liitwalo Hope Raisers, yaani Wakuza Tumaini, kwa hakika mafanikio ya Daniel hadi sasa yamekuwa ya kipekee sana.

Kwa vijana wengi wanaoishi Korogocho, hata kuhitimu elimu ya sekondari bado kwao ni chagamoto. Hata kwa wale wanaomudu kuhitimu masomo yao hakuna faida dhahiri inayotokana na elimu yao katika nchi yenye matarajio madogo kwa vijana. Rushwa, ukabila, ubaguzi, na udhalilishaji vimepenya katika kila nyanja ya kijamii. Kupata kazi hakutegemei sana sifa zao, uwezo wao, au wana juhudi kiwango gani.

Korogocho inatambulika sana kwa sifa mbaya kama moja kati ya maeneo yenye uovu na fujo sana katika mji wa Nairobi ambapo watu huishi maisha yasiyo na utu na umaskini wa hali ya juu, ujinga na kukosa ajira. Wakazi wengi wa eneo hili hawana ajira huku wengine ni vibarua wadogo wadogo viwandani.

Miaka sita iliyopita, Daniel alikaa pamoja na rafiki zake Robert, Isaya na Simon, huko Korogocho na kuanzisha Hope Raisers ili kukuza ubunifu wa sanaa kwa vijana. Kikundi kilianza kwa kutengeneza muziki, na mwaka 2005, Hope Raisers walitoa wimbo kama changamoto kwa viongozi wa Mataifa 8 Tajiri Duniani (G8): "Cancel debts, cancel debts, we are the creditors, why do you want us to suffer? Now you are rich men with our resources." Wenye maana ya "Futa madeni, futa madeni, sisi ni wadai, kwa nini mnataka tuteseke? Mmekuwa watu matajiri kwa rasilimali zetu." Pia, Hope Raisers wanadai kuboreshwa kwa maeneo hatarishi yanayotokana na kutapakaa kwa vilabu, kupita katika njia ambazo hapo mwanzo haikuruhusiwa kupita kwa sababu kuwepo kwa vikundi vya wahuni. Hope Raisers wanajiona kuwa ni mfano wa kuigwa na sura yao mpya inayowakilisha vijana inawaletea heshima katika jamii.



“Mitaa huashiria sehemu muhimu sana ya mwingiliano wa watu na kwa kushawishi watu wa maeneo haya tunaleta mtazamo mpya.”

Kwa mujibu wa Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (United Nations Development Program UNDP), idadi ya vijana wa Kenya inakadiriwa kuwa milioni 9.1 (yapata asilimia 32 ya Wakenya wote), wakifanya asilimia 60 ya nguvu kazi ya taifa. Ingawa kwa ujumla nchi inakabiliwa na kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana ni kilio kikubwa na limekuwa tishio kubwa sana kwa usalama wa watu na wa taifa na kwenye ustawi wa jumla wa jamii.

Korogocho ni makazi ya watu takribani 200,000 wakiwa wamerundikana katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1.5 kaskazini-mashariki mwa Nairobi. Japokuwa kuna uongozi na kituo cha kiongozi mkuu, hamna kituo cha polisi. Polisi kutoka maeneo jirani Kariobangi na Ruaraka ndio hutembelea Korogocho. Wahuni waliokuwa wanatawala Korogocho kwa sasa wamedhibitiwa vyema kuliko ilivyokuwa miaka kumi iliyopita, na wengi wa waliobaki wanafanya uhalifu kwa kificho sana. Jamii imekuwa ikifanya kazi kwa kushirikiana na polisi ili kuzuia vurugu na uhalifu.

Mahali popote duniani ujana ni unatambulika kama kielelezo cha ubunifu, uvumbuzi, maendeleo na tumaini, lakini tumaini hili linapokatizwa ghafla huleta ghadhabu na mtafaruku. Vijana wanaponyimwa fursa na kufanywa masikini, kujiunga na makundi ya uhalifu mara nyingi huwa ndiyo tarajio lao jepesi. Katika maeneo yote ya Kenya makundi ya Mgambo kama vile Mungiki hutoa kitu kama msaada kwa familia na ajira kwa vijana wasio na kazi. Mungiki ni kundi linalojulikana kwa utawala wa mabavu, wakishinikiza raia kulipa ‘kodi’ na kulazimisha utawala wao kwa nguvu na wakati mwingine kwa mauaji. Askari wa Mungiki ni vijana wenye nguvu, wasio na elimu, ajira wala tumaini. Kazi za hila na muonekano wa makundi ya uhalifu hufanya ukweli uliopo kati ya jitihada binafsi za kujikomboa kimaisha na kazi za uhalifu isionekane.

Makundi haya pia huendeleza zaidi ukabila hali ambayo inatishia umoja na mshikamano wa Wakenya. Mungiki lina wanachama wengi wa jamii ya Kikuyu, lakini yapo pia makundi mengine kama Watalibani (hawahusiani na makundi ya waislamu) ambayo yapo chini ya Waluo na Al-shabaab yamekuwa maarufu sana miongoni mwa vijana wa Kenya wenye asili ya Kisomali. Pia tusilifumbie macho suala la utandawazi ambalo limeendelea kuleta

fursa na kupanua wigo kwa makundi ya uhalifu kwa kuleta muunganiko kati ya migambo na jamii za kimataifa. Makundi ya vijana wahalifu ya Kenya hupata wanachama kwa urahisi sana kwa sababu yanaonekana yana ufahamu mkubwa zaidi juu ya uchumi usio halali.

Ni jambo la kukaziwa macho kwamba inakuwaje makundi ya wahalifu yanaonekana kuwa mfano wa kuigwa na vijana wengi na kupewa nguvu ya kudhoofisha na hata kupotosha jamii. Wamekuwa wakitoza kodi zisizo halali, wakijiamulia mambo, wanamiliki silaha ambazo hutumika kufanya vurugu kinyume cha sheria, makundi haya yamechochea uhalifu mijini na vijijini wakati mwingine kwa kusababisha matukio ya mara kwa mara ambayo huleta vurugu kubwa katika jamii. Wakati wa vurugu za baada ya uchaguzi wa mwaka 2008, makundi ya kisiasa yalitumia umasikini na ujinga miongoni mwa vijana kupata vijana wapiganaji kwa kuwalipa pesa kidogo sana kiasi cha shilingi 50 za Kenya (zenye thamani chini ya \$ 1). Kukosekana kwa njia mbadala endelevu za uzalishaji kunaendelea kuvuruga jitihada za kweli za kuleta mabadiliko.

Tofauti na habari hizi, jitihada binafsi ndogondogo kama za kikundi cha Hope Raisers wanatoa njia mbadala kwa kusisitiza

“Mitaa huashiria sehemu muhimu sana ya mwingiliano wa watu na kwa kushawishi watu wa maeneo haya tunaleta mtazamo mpya”

kuwezesha kwa vijana. Hawatafuti misaada ya kifedha toka serikalini, bali wanataka fursa ya kupata huduma muhimu kama vile elimu, huduma za afya, na miuondo mbinu, vitakavyowapa msingi wa wao kujiendeleza wenyewe. Daniel, Simon, Robert na Isaya wana maoni ya kutumia wanachokiita 'uchumi bunifu' ambapo wanaona wana viwekezo vya kuwafanya wajajiri wenyewe kwa sanaa na ubunifu. Haya ni maoni yaliyotolewa na Tom Mboya wa Koch FM, aliyekuwa mfadhili wa Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), anayeendesha kituo cha kwanza cha redio ya kijamii jirani na eneo lilelile. Koch FM inayo milikiwa na kuongozwa na uongozi imara wa vijana, redio hii inatumika kuwezesha na kuendesha mijadala ya kijamii. Pia inafichua mambo maovu yanayotendeka katika eneo husika, na hivyo kupunguza uwezo wa Kiongozi kupokea rushwa na kutoza malipo yasiyo halali kwa wanajamii.

Kwa Tom, suala kubwa ni kuendelea kutengwa kwa vijana kwenye masuala ya kisiasa na kitaifa. Wakati Tume ya Uchaguzi inasema vijana ni asilimia 62 ya wapiga kura wote walioandikishwa, lakini hawana chochote zaidi ya kuwa na nafasi ndogo tu ya ushawishi. Hii haitokani na vijana kutopenda kushiriki siasa na maendeleo. Bali tasnia ya siasa kwa sasa imehodhiwa na kundi dogo la wazee wasomi wenye tamaa ya kujilimbikizia utajiri kwa kuhodhi madaraka serikalini. Kwa makusudi wanawaengua vijana wasishiriki kikamilifu. Watu masikini hasa wa mijini wanaghadhabishwa na uonevu unaofanywa na serikali, hususani vyombo vya sheria ambavyo huwatupia tuhuma vijana na watu masikini. Hivyo kuongezeka kwa utengano kati ya vijana na serikali, pamoja na kukosa kwao tumaini katika

mambo yote kwa ujumla, na hitaji la kupata fursa huwasukumia vijana kujiunga na makundi ya uhalifu. Mpango wa serikali wa kuwezesha utungaji wa sheria pamoja na kukomesha makundi yote ya uhalifu kwa kuanzia mfuko wa ajira na uwezesaji kwa vijana unakaribishwa sana. Ingawa, hatua zaidi zinahitajika kuchukuliwa.

Kuendelea kutumia fedha zaidi kupamba na shughuli za wahuni na vikundi vya uhalifu kwa raia vinavyotishia usalama wa taifa kunaleta umuhimu kwa taifa kubadili mwelekeo na kujipanga upya namna ya kuchukua hatua za kuzuia uhalifu.

Pasipo kuzibwa mwanya uliopo kati ya serikali, jamii na vijana, migogoro, vurugu, utegemezi na kukosa tumaini vitaendelea kuwakosesha fursa vijana. Huenda ni wakati muafaka sasa tuache kawaona vijana kama mzigo kwa taifa na tuwaone ni mtaji wa kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

Wakati umefika wa kufanya mjadala wa kitaifa, ili kushirikisha na kuwajumuisha kwenye nyanja zote za kuleta mabadiliko ya kijamii.

Jaki Mbogo ni Afisa Programu wa Sheria za Makosa ya Jinai na Uhalifu wa OSIEA.



014 SAUTIZETU

KUKATAKATA NA MUMBI NGUGI MAPANGA WATOTO WETU MAUAJI YA WATU WENYE ULEMAVU WA NGOZI (UZERUZERU)

Wakati naandika makala haya, mwili wa mtoto wa miaka tisa, aliyezaliwa akiwa na uzeruzeru, ulionekana pwani ya ziwa Tanganyika, mpakani mwa Tanzania na Burundi, ukiwa umekatwakatwa viungo vyake. Alitekwa huko nyumbani kwao Burundi, na kutolewa kafara kwa imani za kishirikina na tamaa ambayo imekithiri maeneo ya mpakani mwa Tanzania.

Tanzania, na eneo zima la Afrika Mashariki, limehusika na fedheha la mauaji ya kinyama ya watu wenye uzeruzeru, yanayofanywa kwa minajili kuitumia miili yao kwa mambo ya ushirikina. Tangu mwaka 2007, inakadiriwa kuwa idadi ya watu wenye uzeruzeru waliouawa ni zaidi ya 60, wakati mashirika ya watu wenye uzeruzeru kama vile Chama cha Watu wenye Uzeruzeru Tanzania na shirika lisilo la kiserikali (NGO) la Kanada liitwalo Under the Same Sun yanakadiria kuwa idadi inaweza kuwa ya juu zaidi hata kufikia

zaidi ya watu wenye uzeruzeru 100. Idadi kubwa ya watu wenye uzeruzeru, wengi wao wakiwa ni watoto wamebaki vilema maisha yao yote, miguu na mikono yao imekatwa na kutumiwa katika matambiko yanayotangazwa na waganga wa kienyeji kwamba yanaleta utajiri.

Shirika la kijamii la Isaas, lililopo Bukoba, Tanzania, limekuwa likiwasaidia watoto wenye uzeruzeru katika Shule ya walemavu ya Mugeza. Watoto wenye uzeruzeru waliopo katika shule hii ni wahanga wa mauaji ya watu wenye uzeruzeru, wengi wao ni wale ambao wameshakatwa miguu, mikono na watu ambao wameingia mikataba ya uuzaji wa viungo vya watu wenye uzeruzeru kwa waganga wa kienyeji. Wengine wanaishi kwa hofu, hawawezi kuishi maisha ya kawaida kama watu wengine kwa hofu ya kuvamiwa na kuuawa.

Uzeruzeru ni hali ya kuzaliwa ya mapungufu kwenye vinasaba vya ngozi, hurithishwa kutoka kwa wazazi wote wawili, ni hali ambayo hupelekea mtoto kuzaliwa akiwa hana chembechembe (melanin) zinazo zipa ngozi, nywele na macho rangi yake. Kukosekana kwa chembechembe hizi katika ngozi husababisha udhaifu wa ngozi na kuifanya iathiriwe na jua. Pia kukosekana kwa chembechembe katika macho husababisha udhaifu wa macho na hivyo kushindwa kuona vizuri.

Wakati ni vigumu sana kushughulikia aina hii ya ulemavu, changamoto kubwa wanayo kabiliwa nayo wenye uzeruzeru ni kutengwa na kubaguliwa katika jamii. Watoto wenye uzeruzeru hawakubaliki katika mambo mengi, hukataliwa hata na wazazi wao. Hawawezi kupata elimu wala ajira, wengi wao hufanya kazi katika sekta zisizo rasmi na kwenye jua kali. Pasipo kujikinga na jua kwa kutumia vifaa maalum na mavazi marefu ya kukinga mwili, mionzi ya jua hupelekea wao kupata saratani. Wanapokosa huduma muhimu za afya, watu wenye uzeruzeru wengi hufa mapema kutokana na kansa ambayo inaweza kutibika au kuzuilika. Ndiyo maana basi, japokuwa uzeruzeru hauathiri idadi ya miaka yao ya kuishi, ni watu wenye uzeruzeru wachache sana wanoishi zaidi ya miongo minne.

Imani za kishirikina kuhusu watu wenye uzeruzeru zimekithiri. Kwa mfano, inasemekana watu wenye uzeruzeru huzaliwa inapotokea mama mjamzito anajaribu kutoa mimba lakini inashindikana; au mama alishika mimba akiwa katika siku zake za hedhi; pia ni watoto mbadala wa kishetani ambao huwekwa tumboni na shetani badala ya watoto wa kawaida; tena huwa hawafi kama watu wa kawaida bali hutoweka Kimiujiza baada ya kufikia umri fulani. Hata hivyo, imani mbaya zaidi ya kishirikina ni hii ya hivi karibuni, kwamba hirizi iliyotengenezwa kwa kutumia baadhi ya

viungo vya mwili wa mwenye uzeruzeru inaweza kukufanya uwe tajiri, ufanikiwe katika biashara na katika mambo ya siasa. Kwa kadri ilivyozidi kufahamika kuwa na 'thamani kubwa' baadhi ya viungo vya mwili wa mwenye uzeruzeru, kuwa ni mamilioni ya dola, bila shaka ndiyo kilichokuwa kichocheo cha kuongezeka kwa mauaji ya watu wenye uzeruzeru.

Nchini Burundi, serikali ilichukua hatua za haraka sana, kuwakamata mara moja na kuwafungulia mashtaka wauaji. Miongoni mwa mauji 14 walioripotiwa nchini Burundi, 12 kati yake yalipelekea kukamatwa kwa watuhumiwa na kutiwa hatiani. Wakati nchini Tanzania, zaidi ya mauji 63 yaliripotiwa, ni kesi mbili tu ambazo zimepelekea kukamatwa kwa watuhumiwa na kutiwa hatiani. Kuchelewa au kutokuwa na mwitikio kabisa wa kushughulikia matatizo nchini Tanzania, kunaonesha jamii ambayo haijali maisha na haki za watu wenye uzeruzeru. Pia inaweza kuonesha kubanwa kwa sheria na kuhusika kwa vigogo na matajiri katika biashara hii haramu na ya kikatili. Ukubwa wa janga hili dhidi ya haki za binadamu umepita pasipo kuzungumziwa ipasavyo na mashirika ya haki za binadamu. Watu wenye uzeruzeru wananyimwa haki zao za msingi za kijamii na kiuchumi kama vile haki ya kuwa na afya, elimu, na ajira, na sasa wananyimwa haki yao kuu kama binadamu, haki ya kuishi.

Yote haya yanatendeka katika ukanda ambao una mashirika ya kiraia yenye nguvu, na mashirika mengi ya kimataifa ya haki za binadamu. Majukumu muhimu ya serikali na jamii kwa watu (watu wenye uzeruzeru) ni pamoja na kuhakikisha wanapata elimu stahiki, ajira, na huduma za afya, ili kuwawezesha watu wenye uzeruzeru wafurahie haki za binadamu.

Mumbi Ngugi ni wakili wa Mahakama Kuu ya Kenya na Mtendaji wa Shirika la Trustee of the Albinism Foundation of East Africa.



UTO FAU TI UNAPENDEZA

Kwa mtazamo wa Kiafrika, kuzaa mtoto mwenye uzeruzeru inachukuliwa kama adhabu toka kwa miungu na utamaduni zinadai mtoto wa aina hiyo atolewe kafara. Nilikuwa na bahati sikuuawa. Hata hivyo, nilitelezwa na mama yangu akiwa na umri wa miaka 20, ambaye hakuweza kuhimili mzigo wa fedheha na chuki ya alizofanyiwa na jamii kutokana na kunizaa nikiwa na uzeruzeru. Nililelewa na kukua chini ya uangalizi na upendo wa bibi yangu.

WACHA DUNIA IONE ZAIDI YA RANGI YA NGOZI ZETU

Kama ilivyo kwa watu wengi Kenya, hakujua kuhusu hali yangu na matunzo makini yanayohitajika. Kwa nia njema kabisa alikuwa ananiacha juani pasipo kujua madhara yake. Nilipokuwa kijana mdogo nilikuwa nafanya kazi shambani bila kuvaa chochote cha kunikinga dhidi mionzi ya jua. Nilikua narudi nyumbani nimejaa maumivu na malengelenge mwili mzima ambayo baadaye yalibadilika na kuwa mabaka mabaka makubwa. Kwa bibi yangu na jamii nilionekana ni mweupe sana sistahili kuwa Mwafrika.

Shuleni nilikuwa najitenga. Wanafunzi wenzangu walikuwa wananiitaa majina mabaya na kunifuata wakiimba nyimbo za kunidhihaki. Mara nyingi wakubwa walikuwa wanakuja na kubonyeza ngozi yangu. Wengine walikuwa wanaogopa hata kunigusa wakiamini kwamba kwa kunigusa tu wanaweza kupata rangi kama yangu. Niliumia sana moyoni.

Haya yote yamepelekea hata suala la mahusiano binafsi kuwa gumu. Unaweza kumpenda mtu lakini familia, marafiki na jamii wanaweza wasikubaliane. Watasema: Unaidhalilisha familia yao. Baadhi ya wanaume wanakuacha kwa sababu hawawezi kuvumilia maneno ya watu. Wengine wanatokomea kimya kimya bila hata kuaga.

Licha ya miiko na kukataliwa na jamii, baadhi ya watu wenye uzeruzeru wamepambana na kushinda vipingamizi hata kufikia kuwa maprofesa, wanasheria, waalimu, madaktari na wanasiasa wakubwa. Tunafanikiwa kupitia kutetea haki zetu wenyewe. Lakini baadhi yetu tumeshindwa kufika kiwango cha juu kwa sababu ya chuki za kijamii.

Nimekusudia kukomesha mateso ya wenzangu. Tukifanya kazi na asasi ya *Positive Exposure Kenya*, tunatumia picha kama njia ya kuleta mwamko na kubadili mitazamo, hulka na tabia za wanajamii kwa uzeruzeru.

Dunia itazame mbali zaidi ya rangi ya ngozi zetu.

Jayne Waithera ni mwalimu na mjasiriamali anayefanya kazi kama mratibu wa shirika la Positive Exposure Kenya.

TUNASONGEA MBELE KATIKA

Uhamasishaji Wa Jamii Ya LGBTI
Na Nguru Karugu

Kwa jumla, hali ya makundi tengwa ya ngono katika Afrika Mashariki ni ngumu sana na inawadhibiti wahusika kutekeleza haki za msingi za binadamu. Katika kila nchi, bila kuzingatia uanuwai wa dini, imani za utamaduni au mila, kuna chuki dhidi ya wasagaji, mashoga, ngonokuwili, wavukajinsia na mahuntha (LGBTI - lesbian, gay, bisexual, transgender, and intersex)

Kukamatwa kiholela na kutiwa kizuizini, kusumbuliwa na askari wa usalama, vitisho na hongo, dhuluma za ngono na za aina tofauti kutoka kwa polisi, kunyimwa haki za muungano, kufukuzwa shuleni na kubaguliwa katika ajira na makazi, ni baadhi ya kero ambazo huwakumba wanajamii wa LGBTI kila kuchao. Licha ya wingi wa kero wanazopata, mateso haya huripotiwa kwa nadra sana kutokana na hofu ya shutuma na usumbufu unaofanywa na watekelezaji sheria. Kutokana na hali hiyo, ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu dhidi ya jamii ya LGBTI hauripotiwi wala kuwekwa katika kumbukumbu.

Licha ya mazingira haya ya chuki kuu, kumeibuka jamii ya LGBTI iliyo imara, yenye azma na ambayo inanza kukabili uhasama dhidi yao na kudai haki zao kama raia wa kawaida.

William (si jina rasmi), alielezea jinsi genge la wanamgambo lilivyofika nyumbani kwake adhuhuri moja katika mojawapo wa maeneo jirani ya Nairobi. Genge hilo liliwateka nyara William na rafiki yake na kuwapeleka katika eneo moja kwenye bangwa, wakavuliwa nguo na kuanza kupigwa kwa mihimili yenye misumari. Wanamgambo hao walikuwa wamekusanya majina ya watu watakaoshambuliwa na ambao walikisiwa kuwa mabasha. Watishia maisha ya William na rafiki yake ikiwa kila mmoja wao hangetoa kikombozi cha shilingi 550,000 za Kenya (takribani Dola za Marekani 6,500). Baada ya kipigo cha muda na kujaribu kujitetea kwa William, Msamaria mwema aliwaarifu polisi, ambao walifika na kuwakamata wanamgambo hao.

Visa vya hongo kwa raia na polisi vimekuwa vya kawaida. Washukiwa wengi hutoa pesa kwa hofu ya kuitwa wanangono tengwa. Hata hivyo, ili kuonyesha kuwa huu ni wakati wa mabadiliko, William aliamua kuwashtaki washambulizi wake. William - ambaye ni mwandalizi wa kikundi cha afya cha kijamii ambacho kinafanya kazi na wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao (MSM), pamoja na wafanyabiashara wa ngono, kuhusu masuala ya ukimwi na virusi vya ukimwi (HIV/AIDS) - hakutaka kusubiri tena.

Alijipeleka mahakamani na kuwatambua washambulizi wake. Licha ya maombi ya msamaha kutoka kwa familia za watuhumiwa, bado alidai kuwa ni lazima sheria ifuatwe. Kwa sasa, watuhumiwa wako rumande wakisubiri kusomewa mashtaka. William anawakilisha na wakili aliyeajiriwa na Muungano wa Mashoga na Wasagaji wa Kenya (Gay And Lesbian Coalition of Kenya-GALCK) kwa ushirikiano na Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya. William alilazimika kutafuta pesa na kuhamia eneo jingine la mji ili kuepuka mashambulizi mengine na ulipizaji kisasi kuhusu suala la mahakama. Hata hivyo, yeye hajuti alichokifanya na hufika mahakamani kila wakati kesi yake inapotajwa. William anasisitiza kwamba anajivunia kuwa shoga kwani hajafanya kosa lolote la kustahili mashambulizi ya aina hii na anatumai hatua aliyochukua itawazuia wengine dhidi ya tabia kama hizo.

Jamii ya LGBTI ya Afrika Mashariki kama ilivyo kwingineko duniani sio ya jinsi moja. Athari za wavukajinsia, wabadili jinsia na mahuntha, huwa tofauti na zile za wasagaji, mashoga na ngonokuwili. Kuna ukosefu wa ufahamu au ufahamu finyu katika nchi za Afrika Mashariki kuhusu maana ya mvukajinsia. Kuna fasili ya kawaida na inayoeleza kuwa wavukajinsia wanawake huwa ni 'wanaume wanaovaa kama wanawake' yaani mashoga. Hii si sawa, kwa sababu uvukajinsia ni suala la kujitambulisha kijinsia wala si la ngono. Hata matabibu hawajahitimu kukabili masuala kama haya.

Miaka michache iliyopita, mvukajinsia mmoja aliyekuwa na msongo mkuu wa mawazo alienda kwa muuguzi na kuomba aonane na mtaalam wa magonjwa ya akili. Muuguzi yule, alinukuu Biblia badala ya kutumia kitabu cha matibabu, na kumwambia mgonjwa yule kwamba tatizo lake lilitokana na kutofuata neno la Mungu na hakupaswa kulala tena na wanaume wengine. Aliondoka na hakutaka kutafuta tena msaada zaidi hadi mwaka uliofuata alipowazia kujitia kitanzi. Kutokana na hali hii na hali nyingine hasi, baadhi ya wavukajinsia wameasisi shirika la kwanza nchini Kenya la kutetea wavukajinsia na mahuntha. Shirika hili linaendeleza elimu na shughuli za utetezi huku likijaribu kutoa changamoto kuhusu sera za kitaifa zinazoathiri maisha ya wavukajinsia na mahuntha.

Katika mwaka 2009 nchini Uganda, mswada dhidi ya Ubasha (Anti-Homosexual bill au Bahati bill - kutokana na jina la mbunge aliyeuwasilisha) ulipendekezwa bungeni. Mbali na makosa ambayo tayari yalikuwepo katika kanuni ya adhabu, mswada huo ulipendekeza kugeuza na kuongeza adhabu mpya kwa makosa ya ubasha, ubasha uliyokithiri (ambao adhabu yake ni kinyongo), kuendelea ubasha na na kutoripoti mabasha kwa serikali. Zaidi ya hayo, kifungu cha 18 cha mswada huo kilidai “kubatilishwa kwa mikataba ya kimataifa ambayo haiendani na sheria hiyo”.

Muungano wa Mashirika ya Umma kuhusu Haki za Binadamu na Sheria za Kikatiba, umewasilisha kwenye Kamati ya Bunge la Uganda hoja ya kurejelewa upya kwa mswada dhidi ya ubasha kwa vigezo kwamba unakiuka sheria za haki za binadamu za kimataifa na Katiba ya Uganda. Muungano huo umeundwa na wanaharakati wa haki za mashoga pamoja na mashirika ya umma yanayopinga hotuba za chuki, ubaguzi na dhuluma dhidi ya makundi tengwa ya ngono toka kwa wanasiasa, makanisa, na vyombo vya habari. Mswada huu wenye ubishi umewasilishwa mara mbili bungeni bila mafanikio.

Kuwanyima watu haki zao za msingi za binadamu kunaweza kubainisha uzima na kifo. Kituo cha Afrika cha Matibabu na Uhamilishaji wa Wahanga wa Mateso (ACTV) kilicho nchini Uganda kimetoa huduma za matibabu kwa watu ambao wamekuwa wakiteswa na vyombo vya usalama vya taifa kwa kudaiwa kuwa mabasha.

Mwaka 2009, Brian Pande, mwenye umri wa miaka 21 ambaye ni shoga, na Fred Wasukira, ambaye ni mvukajinsia, walikamatwa kwa kutuhumiwa kuwa mabasha. Waliwekwa mbaroni kwa siku 11 kabla ya kufunguliwa mashtaka kwa kukiuka utaratibu asili wa ngono. Kundi tengwa la ngono la Uganda (SMUG) lilitoa msaada wa kisheria na kuwawekea dhamana watuhumiwa hao wawili japo kesi dhidi ya Brian haikuendelea kwa ukosefu wa ithibati. Brian alipigwa vibaya sana na polisi alipokuwa kizuizini na aliaga dunia baadaye akiwa hospitalini akisubiri kesi yake. Asili ya kifo chake haikuwa dhahiri. Inakisiwa kuwa majeraha aliyopata akiwa kizuizini ndiyo yaliyomletea kifo.

Kwa kuzingatia haki ya usiri, hadhi ya mtu, na kuingwa dhidi ya vitendo vya ukatili, mahakama ya Kampala ililiamuru gazeti la “The Rolling Stone” kuwalipa fidia wahusika walioathiriwa na habari kuu ambapo nyuso, majina, makao na maelezo mengine kuwahusu watuhumiwa wa ubasha yalichapishwa pamoja na kichwa cha habari - Wanyongwe.

Mnamo Januari 2011 Mahakama Kuu ililizua gazeti hilo na wafanyakazi wake kuchapisha makala yoyote yanayoleta uchochezi dhidi ya mashoga. Inasikitisha kwamba, hatua za kisheria hazikuchukuliwa haraka kwa David Kato- mwanaharakati madhubuti wa haki za mashoga nchini Uganda ambaye picha zake zilionyesha akiwa amepigwa kwa rungu hadi kufa akiwa nyumbani kwake karibu na jiji la Kampala mwezi Februari 2011. Kifo cha Kato kilikuwa hasara kubwa kwa jamii ya wapigania haki za binadamu wa Afrika Mashariki.

Kampeni kali dhidi ya haki za binadamu za wanajamii wa LGBTI, hotuba za chuki, ubaguzi na dhuluma hudhihirika zaidi katika baadhi ya madhehebu ya Kikristo yanayoungwa mkono na makanisa ya kiinjilisti na viongozi wa dini za Marekani. Wainjilisti watatu wa Marekani: Scott Lively, Caleb Lee Brundidge, na Don Schmierer walifanya kongamano la siku 3 kuhusu ubasha mjini Kampala mwezi Machi 2009. Kanda moja ya video ilionyesha kwamba, Mchungaji Lively anaamini kuwa mashoga walihusika na maangamizi ya kinazi na anaoneshwa akifasili mashoga kama walawiti wa watoto. (<http://www.youtube.com/watch?v=amVnWtpR1is>).

Msimamo mkali kama huo wa kidini, udanganyifu na kutovumilia, unaweza kudhoofisha jitihada za dini nyingine za kukuza uvumilivu, uelewano na ushirikiano. Nchini Uganda, mashirika ya The United Religion Initiative (URI), Great Lakes Chapter, Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), yanajaribu mradi wa mazungumzo utakaojumuisha dini zote ili kuhamasisha na kukuza amani na utangamano katika jamii.

Mifano hii michache ni ishara kwamba watu na vikundi vya jamii ya LGBTI wanaanza kudai haki zao kama raia, na mabadiliko ya kweli na ya kishujaa yatatokea hivi punde katika Afrika Mashariki.

Azimio la Juni 2011 lililopitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu lilionesha shauku kuu na kuagiza uchunguzi ufanyike ulimwenguni kote ili kupata taarifa za vitendo vya dhuluma na ubaguzi unaofanywa kwa misingi ya ngono na jinsia.

Nguru Karugu ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la Public Health Innovations linalolenga masuala ya afya ya jamii na haki za binadamu kwa makundi tengwa ya ngono na jinsia.

“Wafugaji Wa Kikarimojong, wanaoishi eneo hilo, wana elimu duni na makadirio ya umri wa kuishi chini ya wastani wa taifa, huku wengi wakiishi chini ya viwango vya umaskini.”



Wafugaji wa Kikarimojong

021 SAUTIZETU

Na Lochomin Peter Fred

Mtazamo potofu wa Kuwabadilisha Wafugaji Wakikarimojong

Karamoja umebaki kuwa moja ya maeneo lililo nyuma zaidi kimaendeleo nchini Uganda, licha ya jitihada kadha za serikali ya Uganda na mashirika wahisani kujaribu kuliendeleza eneo hilo kame. Wafugaji Wakikarimojong, wanaoishi eneo hilo, wana elimu duni na makadirio ya umri wa kuishi ni chini ya wastani wa taifa, huku wengi wakiishi chini ya viwango vya umskini. Viashiria vya umasikini vinavyoonekana vinatokana na historia ndefu ya kutengwa na kutoshirikishwa kwenye mchakato wa kufanya maamuzi. Hali hii imetokana na ukweli kwamba jitihada za kuendeleza eneo hili zinalenga kubadili mfumo wa maisha yao kama jamii ya wafugaji bila kupewa njia mbadala ya kuendelea na maisha ya ufugaji.

Wafugaji wa Kikarimojong, bado wanaishi kwa kufuata mila za wahenga wao ambazo zinaambatana na ufugaji wa ng'ombe. Kwa kawaida, wanaume ndio hupeleka mifugo malishoni aidha wakati wa msimu au kwenye maeneo yenye hifadhi ya malisho, huku

wanawake na watoto wakibaki katika makazi ya muda na kuangalia masuala ya nyumbani. Kutokana na mabadiliko ya misimu katika ukanda huu, mifugo inahitaji kuhamishwa wakati wa ukame kwenda sehemu yenye maji ili kuhakikisha wanapata malisho ya kutosha na kuongeza kiwango cha kuzaliana. Nyakati za ukoloni, eneo la Karimojong liligawanywa ili kuweka mipaka ya kimataifa ya Uganda, Kenya na Ethiopia. Mipaka hii inakatiza maeneo ya panda za malisho ya zamani ya Wakarimojong, tangu kuwekwa kwa mipaka hiyo kumekuwepo na migogoro ya mara kwa mara maeneo ya mipakani, ikihusisha uporaji wa mifugo na vurugu zisizoisha. Sehemu nyingi nje ya Karimojong, vurugu na wizi wa ng'ombe vimekuwa ndiyo utambulisho wa Wakarimojong, lakini hali hii ya vurugu sio utamaduni wa Wakarimojong. Kabla ya ardhi yao kugawanywa chini ya utawala wa kikoloni, wafugaji walikuwa wakipora na kuibiana ng'ombe. Huu ulikuwa ni utamaduni wao, ambapo mapambano na uporaji wa mara kwa mara ulipelekea kugawanyika

“
**Tangu mwaka 1911
Wakarimojong
wamekuwa wakiachwa
katika michakato ya
utungaji sera uandaaji
wa mipango na
utekelezaji wa sera**
”

kwa ng'ombe kwa wanajamii. Uporaji huu wa ng'ombe ulikuwa wa kutumia mikuki, sio bunduki. Bunduki zimeanza kutumika katika ukanda huu kwa sababu ya migogoro ya majirani Somalia, Kenya na Sudani. Uporaji wa ng'ombe wa siku hizi ni wa mapambano makali na ng'ombe wanaporwa ili kwenda kuuzwa sio kupelekwa vijiji vingine. Bwana Ekasikout Apaaloculur, wakati wa mkutano wa hadhara wa wafugaji wa Kangole, alielezea jinsi alivyolazimika kuyakimbia makazi yake kwa sababu ya kukosa usalama, ambapo vijana walifanya ghasia, kuuu watu, kupora na kubaka wanawake. *“Mji wangu umekuwa pango la majambazi na si salama kwa yeyote”*

Majibu ya serikali na wabia wa maendeleo kuhusu tatizo la eneo hili imekuwa ni kujaribu kuwaelimisha ‘kuwastaarabisha’ wafugaji, kubadilisha mifumo ya maisha yao, mana kwa mtazamo wao ufumbuzi wa amani ya kudumu katika mkoa huu ni kufuata mfumo wa sasa wa maisha. Muda mwingi kumekuwa na jitihada ndogo sana za kuelewa mahitajiya kipekee ya wafugaji wa Karamojong. Tangu mwaka 1911 Wakarimojong wamekuwa wakiachwa katika michakato ya utungaji sera, uandaaji wa mipango na utekelezaji wa sera. Mara baada ya kupata uhuru serikali haikufanya jitihada za kutosha kufuta mwendelezo wa sera zinazowabagua kwenye maendeleo wafugaji

na makundi ya jamii za watu wachache katika eneo la Karamoja, na hivyo kuvuruga uzalishaji wa wafugaji ka tika eneo hilo. Inaonyesha kuwa wadau wote hushiriki na kuchangia katika mipango inayowahusu wao pia. Ikumbukwe kuwa kukosekana kwa taasisi maalumu inayotoa taarifa na ushauri kuhusu masuala ya wafugaji imesababisha jamii za wafugaji kuonekana kama tatizo badala ya watu wenye mahitaji maalumu ya maendeleo. Kwa hiyo, hali iliyoozoeleke ni kwamba ufumbuzi lazima utoke nje na hivyo wanalazimisha wafugaji kubadili mifumo ya kuishi, kuelimika, kupunguza mifugo, kulima na kulima mazao na wanazuiwa kuhamia maeneo ya jirani na kwenye hifadhi za taifa. Hivyo, mifumo yote ya maisha miongoni mwa jamii za Karimojong yanayotengenezwa na watu bila kufuata mabadiliko ya asili.

Sehemu kubwa ya ardhi inayokaliwa na wafugaji ni ardhi asili, ilitolewa chini ya Sheria ya Ardhi ya Uganda ya mwaka 1998. Hii ina maanisha kuwa ardhi humilikiwa na ukoo kwa pamoja, na ukoo unajukumu la kusimamia umiliki, matumizi na urithi wa ardhi hiyo kwa wahusika. Kwa mujibu wa ripoti ya shirka la SOS Sahel UK, serikali ya Uganda inataka kuleta ufumbuzi wa migogoro katika eneo Karamoja kwa kuhamasisha uwekezaji kutoka nje. Katika harakati za kuwanyang'anya silaha wafugaji, kunafanyika uharibifu na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kuna taarifa kwamba kampuni moja la kigeni (bio fuel feedstock) linafanya majadiliano na serikali kuchukua ardhi ya wafugaji kwa kuendesha

shughuli binafsi za kilimo. Wakarimojong hawataki kuona serikali ya Uganda ikitumia nguvu kuwapokonya ardhi kama ilivyotokea mwaka 2005 kunajirudia tena, ambako kulipingwa na mashirika mengi ya haki za binadamu ikiwemo Tume kuu ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (OHCHR), kufuatia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanywa na askari wakati huo.

Ili kubadili hatua za kuendelea kuitenga na kutoishirikisha jamii ya Wakarimojong kwenye mipango ya maendeleo, Mradi wa Sheria ya Wakimbizi 'Refugee Law Project (RLP)' umejenga ofisi za utafiti na utetezi katika mkoa wa Karamoja. Ofisi hii imekusudia kuendesha utafiti ambao utaonesha uhalisia wa maisha katika eneo la Karamoja kwa ujumla. Pamoja na hayo, inakusudia kuandaa jukwaa la wakaazi kupaza sauti zao kwa watunga sera na wafanya maamuzi kuhusu kero wanzokumbana nazo. Mradi una lengo la kubadili picha na mwonekano mkoa wa Karamoja ulizoeleka wa kitaifa na hata nje, na kuhamasisha umuhimu wa kuchukua hatua sahihi na za haki kila wakati inapohitajika kufanya hivyo. Hatua zinazozingatia haki zitaweka mbele maslahi na haki za wafugaji kwa kila mpango wa maendeleo unaoanzishwa eneo hilo.

“Tumebaki kuwa watu wa kupokea tu, ni kama shimo la takataka kwa wote; fulani na fulani wanakuja wanatupia hapa, wengine wanakuja, wanafanya vilevile kama wa kwanza, tufanye nini mwanangu? Tumekuwa sehemu ya kuchumia kwa

mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), wanakuja wanatudanganya na kula mali yetu; hatujawahi kuhusika katika miradi wanayoleta. Mara nyingi tunaandikishwa majina kila kaya lakini hakuna tunachopata; sidhani kama hali hii itaisha hivi karibuni, natoa wito kwa viongozi wetu watulinde na unyonyaji huu”, Mzee Lopunoole Zachariya wa Kraal karibu na Mji wa Nakapiripirit (mwezi Julai 2010).

Mashirika ya RLP, Changing the Lens (CTL) inahitimisha kwa kutambua kwamba mkoa wa Karamoja pamoja na wakazi wake walibaguliwa katika historia nzima ya ukoloni na baada ya uhuru. Kubaguliwa huku kumesababisha sio tu umasikini, bali pia kulifanya eneo zima kuwa nyuma sana kimaendeleo na kuhitaji aina mbalimbali za uongozi ili kulifanya lisonge mbele na kufikia kiwango cha maendeleo sawa na maeneo mengine nchini. Vilevile mikakati maalumu ya maendeleo, ikiwemo inayohamasisha kuacha mapigano na maisha ya kuhamahama, imebuniwa kwa namna ambayo haizingatii utu, haki, siasa, maendeleo ya kiuchumi ya jamii husika iliyoathirika, hali ambayo inaleta upinzani na kupoteza tumaini kama kweli serikali ina nia ya dhati kupanga kwa maslahi ya jamii ya wakaramajong.

Lochomin Peter Fred ni Mratibu wa Utafiti na Utetezi wa Mradi wa Sheria ya Wakimbizi, Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Makerere tawi la Karamoja.

W A N A W A K E N C H I N I U G A N D A



Wakati wowote tunapotembelea Kituo chetu cha Afya cha II ili kupata huduma, hatujawahi kuwapata wafanyakazi watatu wa afya tuliombiwa wamepangiwa kituo hiki. Badala yake, maelezo na tiba ikiwemo kuchoma sindano-hufanywa na mlinzi na bawabu kama vile na wao wamesomea kazi hiyo....Kibaya zaidi, hufungua kituo pale wanapojisikia. Siku wakiwa na furaha, watafungua ofisi muda ambao wao wanaona ni mapema sana saa 4:00 asubuhi, vinginevyo hufungua ofisi mchana na kufunga saa 9 alasiri. Wakati mwingine hutupa adhabu tunapochelewa na kufika saa 8:00 mchana. Na adhabu zenyewe inabidi tuwachotee maji japo safari mbili ili tupate huduma....

Atim Leah Perpetua, mwenye umri wa miaka 38 Mwanamke wa Uganda Kaskazini, anaeleza kero yake kuhusu Kituo cha Afya II cha Abunga katika mdahalo wa jamii (Mwezi Machi 2010)

Wanawake Hujenga Kundi Muhimu Kuleta Mabadiliko na Eunice Apio

Kituo Cha Afya Cha Abunga II, kama ilivyo pia kwa vituo vingine vya afya 142 vyenye mazingira yanayofanana, kinapatikana katika eneo lililoathiriwa na vita la Lango, Uganda Kaskazini. Eneo hili limeharibiwa na Majeshi ya Upinzani ya Waasi (Lord Resistance Army), ambayo yameharibu na kuteketeza Uganda kaskazini kwa miaka zaidi ya ishirini. Baada ya vita, jamii zilizokimbia makazi yao zinarudi na kukuta miundombinu michache au hakuna miundombinu wala huduma za kijamii.

Wanawake wanakabiliwa na mzigo mkubwa wa kujenga upya masalia ya familia na jamii zilizoathiriwa kiuchumi na kisaikolojia. Kukithiri kwa ulevi kwa wanaume, kukosa ajira, na ukatili majumbani ni vitu vya kawaida. Pamoja na hali hii, bado wanawake wanaokota vipande vya mabaki na kujenga upya maisha yao. Wanabeba majukumu makubwa ya kuzalisha chakula na kutafuta chakula, kufuata maji umbali mrefu, na kuhakikisha watoto wao wanakwenda shule. Wanaishi katika dimbwi la umasikini mkubwa, wanapata msaada kidogo sana au hawapati kabisa msaada toka serikalini.

Eneo la Atim linakadiriwa kuwa na idadi ya watu 1,751,050 kwa mujibu wa takwimu za sensa ya mwisho ya mwaka (2002) kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa ya Uganda. Katika idadi hiyo, asilimia 51 ni wanawake wenye umri zaidi ya miaka 15.

Kudhoofika kwa idara ya afya ni moja ya mifano ambayo serikali inashindwa kutekeleza majukumu yake. Hali inazidi kuwa mbaya kwa sababu ya serikali ya Uganda kupuuzwa baadhi ya maeneo, kama ilivyotelekeza eneo la kaskazini; kutojali kwa watendaji wa serikali za mitaa ambao wanashindwa kusimamia na kutoa huduma za kijamii,

na kushindwa kwa muda mrefu kwa serikali kuu kutekeleza kwa vitendo ahadi zake za kujenga Uganda Kaskazini.

Matokeo yake ni kwamba, mwanamke wa kawaida wa Uganda kaskazini anakabiliwa na mambo makubwa matatu; hatari ya kuuawa kutokana na migogoro ya baada ya vita, umasikini wa kupindukia (takwimu za umasikini wa Uganda Kaskazini zinaonyesha kuwa ni asilimia 64 tofauti na wastani wa taifa ambao ni asilimia 34 kwa mujibu wa Kituo cha Utafiti wa Sera za Uchumi Uganda na Ofisi ya Takwimu ya Uganda 2003) na kukosa uwezeshwaji kabisa.

Serikali imetangaza mchakato mkubwa wa Amani, Urejesho, na Maendeleo (Peace, Recovery and Development Program 'PRDP') unaoonyesha jitihada za kuiimarisha na kuirejesha Uganda Kaskazini ndani ya kipindi cha miaka mitatu ijayo kwa kupitia mipango mbalimbali itakayosimamiwa na kuendeshwa kwa pamoja. Wadau wote ikiwemo wahisani wa maendeleo wanatakiwa kuingiza program zao katika mpango huu. Jitihada za ujenzi mpya baada ya mapigano, tayari umeshagharimu mabilioni ya dola.

Kwa bahati mbaya, mpaka sasa hakuna chochote kinachooneka kufanyika katika eneo hili, kutokana na usimamizi mbaya wa fedha unaofanywa katika ngazi za viongozi wasimamizi, kutokuwajibishwa kwao ambako kunaendelea kuwaneemesha viongozi wabaya na ukimya wa wananchi kutohoji wala kufuatilia kinachoendelea.



WANAWAKE KUSHIKA HATAMU


FAPAD ni shirika lisilo la kiserikali la Uwezeshaji Amani na Maendeleo lilipo eneo la Lango, linasaidia kuziwezesha jamii wahanga wa mapigano kwa kushirikiana na PRDP, ambalo pia lipo chini ya Azimio na 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake, Amani na Usalama; Kwa msaada OSIEA-, Open Society Foundations programu ya Kimataifa ya wanawake, FAPAD inatumia mwongozo wa PRDP kama fursa ambayo inaweza kutumiwa vizuri kuchochea kuwezesha kwa wanawake kiuchumi na kushiriki katika kujenga upya mkoa huo.

Habari hii ya mabadiliko tayari imekwishaanza. Mwanzoni, wanawake hawa waligundua kuwa hawakuwa na ujuzi wala taarifa za kuwawezesha kushiriki kikamilifu kama wazalendo na wanaoweza kusukuma utawala bora. Lakini sasa wanatambua kuwa mabadiliko yanaanza na wao wenyewe kwanza. Ni lazima watengeneze fursa na kuzitumia kufanya maamuzi ya maana katika ngazi zote ili mambo yafanyike. Ndio maana, mwezi Agosti 2009 wanawake vijijini wapatao 800 wao walifanya uwezeshaji maalum wa kiraia kwa vikundi 20 vya kiraia mkoani kote. Mwaka mmoja baadaye, wanawake hawa wa vijijini walihamasisha kikamilifu wanawake wenzao kuungana nao ili na kudai wasikilizwe katika kufanya maamuzi ili waweze kushiriki vizuri kuujenga upya mkoa wao.

Kupitia elimu, mijadala, hati za madai, na maandamano ya amani, wanawake hawa wamefanikiwa kurejesha hadhi ya kituo cha afya cha Abunga II. Kuna kundi linaloongezeka miongoni mwao ambalo linaratibu ubora wa huduma zinazotolewa na wafanyakazi katika vituo vya afya kwa mujibu wa viwango vya serikali na kudai vituo viboreshwe. Pia wanafuatilia kwa karibu shule za msingi wanazosoma watoto wao, wanakagua utoro wa walimu na kuhoji matumizi ya pesa za shule. Zaidi sana, wanashiriki kwa karibu katika kuratibu kikamilifu ujenzi wa barabara, shule na vyanzo vya maji ili kuondoa umasikini katika maeneo yao. Wanawake pia waanzisha “ufumbuzi kuanzia nyumbani” mkakati wa kukabiliana na masuala muhimu ya kijamii kama vile unyanyasaji wa kijinsia, ambao kwa bahati mbaya imebaki kuwa moja kati tatizo kubwa la uvunjaji wa haki za binadamu katika eneo hili.

Kilichobakia ni kuimarisha mafanikio haya na kuyaendeleza zaidi ili kuongeza idadi yao na kufikia wanawake makini 8,000,000 wenye shauku kubwa na waliotayari kuleta mabadiliko ya kudumu katika Mkoa wa Lango.

Eunice Apio ni Mkurugenzi wa Asasi ya FAPAD iliyoko Uganda Kaskazini.

A close-up photograph of a person's face in profile, wearing glasses, looking out a window. The window has a grid pattern. A hand is visible in the foreground, with fingers pressed against the glass. The background outside the window is a bright, hazy sky. The overall color palette is dominated by warm yellows and oranges, transitioning to cooler blues and greens near the window.

KUFUNGIWA

NDANI

WATOTO WENYE ULEMAVU WA AKILI NCHINI KENYA

Na Emma Day

Katika nyumba nyingi maeneo yote ya Kenya, watoto wanafungiwa ndani, wanafichwa wasionekane katika jamii, wakati mwingine hufungiwa kwenye samani ili kuwazuia wasiweze kutoroka. Watoto hawa ni wenye ulemavu wa akili (utahira), ambao kama watoto wengine huzaliwa na matatizo ya akili. Nchini Kenya watoto wa aina hii hawaeleweki katika familia zao na jamii zao, hali inayopelekea hofu, unyanyapaa na kubaguliwa

Kuna uelewa mdogo sana kuhusu ulemavu wa akili nchini Kenya, na kwa imani za kijadi tatizo hilo linaashiria kuwepo kwa laana au kurogwa, na au malezi mabaya ya wazazi. Utaahira ni ugonjwa unaokua, unaanzia wakati wa kuzaliwa, na una sifa za kumfanya mtoto kutofurahia jamii, kushindwa kuongea vizuri, kutoa lugha za matusi, mihemko ya ghafla, na tabia za ajabu ajabu.

Chama cha Watu Wenye Ulemavu Akili cha Kenya (The Kenya Association for the Intellectually Handicapped-KAIH) kinaripoti kwamba Kenya Magharibi katika maeneo ya Nyanza, kuna utamaduni kwamba mtu anayekufa katika mazingira ambayo wanaamini kuwa ya 'unajisi' hufanyiwa 'ibada ya kutakaswa'. Ibada hii huambatana na kumlazimisha mtu mwenye matatizo ya akili kufanya ngono na maiti.

Watu wenye matatizo ya akili nchini Kenya bado wanahangaikia kupata haki zao za msingi za kibinadamu kama kupata elimu na huduma za afya. Wanabazwa katika jamii na kunyimwa haki kamili za uraia na kuwa na uhuru wa kuamua katika mambo yanayogusa maisha yao. Chini ya Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD), ambao Kenya iliridhia, watu wenye ulemavu wa akili wanastahili kupata haki kamili za binadamu sawa haki za watu wasio na ulemavu.

Briana ana umri wa miaka 24 na ana ulemavu wa akili. Baada ya kumaliza shule ya msingi alijiunga na mafunzo ya ufundi ambako alijifunza kozi ya matumizi ya kompyuta, lakini hakupokea cheti chochote. Baada ya hapo alienda kujiegesha akisaidia kazi katika duka moja la kompyuta kwa miezi mitatu, lakini hakupewa kufanya kazi yoyote muhimu, hivyo alitumia muda wake mwingi kufuta vumbi na kucheza michezo ya kwenye kompyuta.

redio mbovu na aliambiwa atapewa mafunzo zaidi. Kazi hii haikwenda vizuri kwa sababu wafanyakazi wenzie walijibagua na kumwacha Brian peke yake bila kupewa mafunzo yoyote. Kutokana na hali hiyo, Brian hakutarajiwa kufanya chochote zaidi ya kufagia ofisi na kukaa bure. Brian aliacha kazi hiyo na sasa anatumia siku mbili kwa juma akiwa KAIH akijifunza ujuzi wa mambo ya ofisi, na muda mwingine wote hubaki amekaa nyumbani peke yake akiangalia TV na kusikiliza muziki. Brian anapenda baadaye angefanya kazi hospitali kitengo cha maabara, lakini haoni tumaini juu ya hilo kwa sababu anahisi watu hawatambui jinsi alivyo. Hajisikii vizuri kumtegemea mama yake kwa kila kitu, na anatamani kuwa na uhuru zaidi.

Hali ni tofauti kwa Felicity Ngungu ambaye mjukuu wake alikuwa na ulemavu wa akili, hapakuwa na taarifa zozote wala dalili za utaahira kwa mjukuu wake tangu kuzaliwa kwake miaka 28 iliyopita. Alipogundua kwa mara ya kwanza mambo anayofanya mjukuu wake kwa watoto wengine sio ya kawaida, alimchukua na kumpeleka kwa madaktari mbalimbali, wote walimwambia mjukuu wake amechanganyikiwa, na ampeleke hospitali za watu wenye matatizo ya akili. Felicity aliweza kujua kuhusu utaahira kupitia profesa mmoja kutoka Uingereza ambaye alikuja kutembea na pia kupitia ndugu wengine walioko Marekani, na kwa kutumia uelewa huo alianzisha Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Akili Kenya (ASK).

Kwa sasa tayari ASK inapokea msaada kutoka Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA) na Mental Health Initiative

ya shirika la OSF. ASK inatoa msaada kwa familia zenye watu wenye ulemavu wa akili, na inawasaidia kupata huduma za uchunguzi wa kitabibu wa afya zao. Kupitia ASK, Felicity ameweza kupata fedha kwa ajili ya kugharamia kituo maalumu cha watoto wenye ulemavu wa akili cha shule ya Msingi City mjini Nairobi. Kwa ujumla hata pale ambapo watoto wenye udhaifu wa akili wanajumuishwa katika mikondo ya shule za kawaida, wakihitimu darasa la 8 hawapati vyeti kama ilivyo kwa watoto wengine. Wakifika darasa la 8 ukifika wakati wa mitihani ya mwisho, huambiwa warudi nyumbani. Kitendo hiki ni kuwanyima haki yao ya kufanya mitihani kama wenzao, shule huwakatalia kufanya mitihani kwa sababu wakifanya wanasababisha shule ishuke wastani wa mwaka wa kufaulisha wanafunzi. Bila cheti cha shule ya msingi huwezi kujiunga na elimu ya sekondari.

Ulemavu wa akili na umaskini ni chanda na pete; vinaenda pamoja. Ulemavu unaweza kusababisha umaskini katika familia kwa sababu ya gharama kubwa za matibabu, usafiri, na muda wa kuwahudumia. Kwa ujumla hali ya ulemavu bila rasilimali huwa mbaya zaidi, hutengeneza duara la umaskini na udhaifu usiopungua. Kwa watu wenye ulemavu, gharama za kupata elimu ziko juu sana, na mara nyingi familia huwa hazioni umuhimu wa kusomesha mtoto mwenye ulemavu. Ni kawaida kabisa kwa mtoto mwenye ulemavu kuwa wa mwisho kupelekwa shule au hata kununuliwa nguo katika kila familia, kwa sababu mahitaji yake mengine yatapewa kipaumbele zaidi.

Asasi zote ASK na KAIH, pamoja na OSIEA zinaripoti kwamba kupata huduma za

afya kwa watu wenye ulemavu wa akili, ikiwemo wenye utaahira ndiyo jambo gumu zaidi. Wataalamu wa afya hawalitambui vizuri tatizo hili. Mara nyingi wataalamu wa tiba, huwaambia wazazi wawapeleke watoto wenye utaahira kwenye taasisi za watu wenye matatizo ya akili kwa sababu 'ni vichaa'. KAIH iliendesha uchunguzi ulioonesha kwamba, watu wengi wenye matatizo ya akili hufa kabla ya kufikisha miaka 30. Mara nyingi madaktari hupuuza kutibu dalili ndogondogo zinazojitokeza kwa mgonjwa wa akili, ambazo hupelekea kukua kwa ugonjwa kusiko kwa lazima, hali kuendelea kuwa mbaya hadi kifo. Wakati wa zoezi la uchunguzi wa mahitaji ya watu 122 wenye matatizo ya akili lililoedeshwa na KAIH, watu 50 walipatikana na magonjwa ya zinaa yasiyotibika. Binti mmoja alikutwa mjamzito na ana Virus Vya Ukimwi na hakuwa anajua lolote kuhusu hali yake. Kwa ujumla jamii na wataalamu wanaokutana na watu wenye ulemavu hufikiri hawana hisia za kujamiana. Kudhani hivyo, ni sehemu ya ukatili, huleta mwanya wa kufanyiwa vitendo vibaya vya ngono kwa watoto wenye ulemavu wanaokuwa.

Shirikisho la mashirika ya afya na haki za binadamu, likiwemo shirika la Open Society Foundations, wanaanzisha kampeni ya kukomesha ukatili katika vituo vya afya. Aina ya mahusiano yanayojitokeza kati ya watoa huduma za afya na watu wenye matatizo ya akili ambayo ni sawasawa katika maeneo yote Kenya, imetawaliwa na matusi, ikiwemo kuwatuhumu ni vichaa, kulazimishwa kwenda katika taasisi maalum za walemavu, au kunyimwa matibabu. Hii huzidisha ukatili na udhalilishaji, na

Watu wenye ulemavu wa akili nchini Kenya bado wanahangaikia kupata


wakati mwingine huteswa. Kwa habari zaidi na kuchukua hatua za kukomesha ukatili katika vituo vya afya, fungua tovuti ya www.stoptortureinhealthcare.org

Watu wenye ulemavu wa akili nchini Kenya, sawa na watu wenye ulemavu mwingine, wameachwa na kubaki nyuma katika jamii. Katiba mpya ya Kenya ya mwaka 2010 inatoa fursa kwa mawakili na wanaharakati kutetea haki zao. Pongezi za shukrani kwa utetezi unaofanywa na mashirika kama vile ASK na KAIH, taratibu mitazamo ya wanajamii imeanza kubadilika. Tume ya Taifa ya Haki za Binadamu nchini Kenya, ambayo ni chombo cha serikali kinachoshughulikia haki za binadamu mwezi Januari 2011 kimeanzisha Kituo cha Walemavu, mradi unaohusu utetezi wa haki za watu wenye ulemavu. Pamoja na hatua hizi, bado tuna safari ndefu kuwasogeza karibu watu wenye kupata haki sawa.

Emma Day ni Mwanasheria wa kujitegemea aliyeko Nairobi, Kenya.




haki zao za msingi za kibinadamu, kama vile elimu na huduma za afya





**Kuhimiza midahalo
elimishi katika
*mijadala ya umma***



WATU WAFUPI WAFUPI

Umbilikimo ni ule mkusanyiko wa hali za maumbile inayoleta ufupi kuliko kawaida katika ukuaji wa mifupa ya mwili (urefu usiozidi futi 4 na inchi 10). Kuna zaidi ya hali 200 zinazoweza kusababisha umbilikimo, na kila hali ina sifa zake tofauti.

KUPAZA SAUTI: UMBILIKIMO | NA ANNET NAKYEYUNE

Umbilikimo ni hali ambayo haieleweki vizuri kwa watu wengi, na yenye changamoto za kijamii, kitabibu, na kimazingira kwa watu ambao wameathiriwa na hali hiyo. Umbilikimo ni ule mkusanyiko wa hali ya ufupi kuliko kawaida ya ukuaji wa mifupa ya mwili (urefu usizidi futi 4 na inchi 10). Kuna hali zaidi ya 200 zinazoweza kusababisha umbilikimo, na kila hali ina sifa zake. Sifa ambayo ipo katika kila mbilikimo ni kwamba, ni watu wazima lakini wafupi sana kuliko wastani.

Kwa watu ambao wameathiriwa na umbilikimo, ubaguzi huanzia nyumbani, huitwa watu wadogo wadogo. Hujikuta hawakubaliki katika familia zao hasa baba na ndugu. Akina mama hulaumiwa na kutelekezwa kwa kuzaa mtoto mbilikimo katika familia.

Pengine cha kushangaza wakati naandika makala haya, akina mama ambao ni watu wafupi wafupi miongoni mwa jamii ya watu

wafupi wafupi wa Uganda (Little People of Uganda- LPU) walikuwa na watoto wenye urefu wa wastani wa wanaume wa kawaida. Jenifer anasema kwamba wanaume wa kawaida huzaa na mbilikimo lakini hawataki kuwaoa: “Mahusiano yetu hufanyika gizani tu. Wanawakataa watoto ambao tunazaa nao kwa sababu ya kuogopa kero na kuchekwa na wanafamilia na pia jamaa zao.” Kwa wale ambao baba zao “huwakubali”, bado hukabiliwa na changamoto ya kukubalika na kupewa ushirikiano katika familia zao. Kwa mfano, kuna mwingine, kila ikitokea baba yake akiulizwa ana watoto wangapi alisema: “Ningekuwanao watano lakini mmoja wao ni batili”. Hii ina maana mtu huyu hakuwa akichukuliwa na baba yake kama binadamu aliyekamilika. Ziwa ambaye ni mtu mfupi alitumia maisha ya utoto wake yote akiwa kafungiwa ndani ya ngome kwa sababu baba yake alikuwa anaogopa kuchekwa na wenzie na hata majirani zake kutokana na hali isiyo ya kawaida ya mtoto wake.

“

Mahusiano yetu hufanyika gizani tu. Wanawakataa watoto ambao tunazaa nao kwa sababu ya kuogopa kero na kuchekwa na wanafamilia na pia jamaa zao.”

”

Kwa sababu ya uelewa mbaya na unyanyapaa, watoto wengi wa aina hii hawapelekwi shule. Wazazi sio tu wanatilia mashaka uwezo wa akili za watoto wao, lakini pia wanaamini kuwa hawawezi kupata kazi za kitaaluma. Hii inatokana na kuenea kwa imani kwamba mbilikimo wana muonekano wa kilemavu hivyo wanafaa katika mambo ya burudani tu, na kwa hakika wengi wao wameajiriwa katika eneo hilo. Mara nyingi mbilikimo wanapokwenda kutafuta ajira, huambiwa waziwazi kwamba hawana uwezo wa kufanya kazi, pia hawawezi kuheshimiwa na wateja au wabia wao. Watoto wenye umbilikimo hawaachwi katika hili; hutumika kama wachekeshaji kwenye matamasha. Pamoja na hayo, baadhi ya shule binafsi hazibandikishi watu mbilikimo, na huwashauri wazazi wawapeleke watoto wao kwenye shule maalumu. Hata hivyo, kama ilivyo kwa mbilikimo watu wazima, hata watoto walioathiriwa na umbilikimo sio wote wanamahitaji maalumu. Wanachohitaji ni matunzo mazuri ya kawaida ambayo yatawawezesha kuendana na jamii ambayo imejengwa kwa kufuata hali ya watu wenye urefu wa wastani. Kwa mfano shuleni wanaweza kutengenezewa ngazi za kupandia ili waweze kufikia vitabu katika mashelfu ya maktaba, na kufikia vyoo n.k.

Budalah aliacha kuendelea na shule kwa sababu ya miguu yake kufa ganzi kulikotokana na saizi kubwa ya viti: “Kilichokua kinatokea ni kwamba nilikuwa nikisimama naanguka na watoto walikuwa wanaogopa wanasema nina kifafa. Walikuwa wanajitenga”. Kama ilivyo kwa watu wengine wenye ulemavu, watu wafupi wanachangamoto ya kupanda kwenye majengo na vyombo vya usafiri, hasa mabasi. Hali hii inawafanya washindwe kutumia vizuri uwezo wao. Utafiti mdogo uliofanywa

hivi karibuni na asasi ya LPU umegundua kwamba sheria nyingi za serikali ya Uganda zinazohusiana na elimu, usafiri, maktaba na afya haziwagusi wala kuwasaidia watu wanaoishi na ulemavu. Kutokana na Azimio la Kimataifa la Haki za watu wenye Ulemavu serikali ya Uganda inapaswa kuhakikisha kuna usawa wa kupata huduma kwa walemavu, wakiwemo mbilikimo.

Katika jamii ya Uganda watu wafupi wanachukuliwa kama “mali ya umma” na kila mtu anajiona ana haki ya kutoa maoni, kubeza, kutukana, kushambulia mtu mfupi. Sio jambo la kushangaza kukuta watu wakizingira, wakimcheka na kumwita majina ya dhihaka mbilikimo anapopita. Mwanachama mmoja wa asasi ya LPU aliacha kazi yake ya biashara ya uchuuzi kwa sababu watu walikuwa wakimzingira, wanamshangaa, wanamcheka na kumwita majina kwa utani. Pamoja na hayo yote, japokuwa watu walemavu wa Uganda wanatambulika katika mambo yote kwa ujumla, mbilikimo wanabaguliwa hata miongoni mwa jamii ya walemavu. Ni lazima kuwekwe msisitizo kwamba, kama ilivyo kwa watu wengine katika jamii, watu wafupi na mbilikimo wanahitaji kupendwa na kuheshimiwa. Wanahitaji kutambuliwa kuwa ni miongoni mwa makundi ya watu wenye ulemavu.

Udhhalilishwaji mara nyingi unaweza kuwa kimwili au wa maneno. Udhhalilishwaji wa kijinsia imekuwa ni kawaida kwa mbilikimo ambao hufanyiwa hayo kwa sababu ya maumbo madogo ya miili yao na mara nyingi kwa sababu hawathaminiwi katika jamii. Nakayiwa alidhalilishwa kijinsia mara kwa mara na vijana na wanaume wakubwa kwa sababu hakuwa anaweza kujilinda mwenyewe: “Walikuwa wanavivizia

nikiagizwa na mlezi wangu kwenda kuchota maji au kutafuta kuni. Walikuwa wananivua nguo na kusema wanataka kunithibitisha kama ninafanana na wanawake wengine. Wananibaka na kukimbia. Lakini nilikuwa nikimwambia mlezi wangu kuhusu ninayofanyiwa alikuwa hajali”.

Pia mbilikimo wanakabiliwa na hatari ya kuuawa wangali bado wadogo, kwa sababu sio jambo geni kwa familia nyingi kuwauwa watoto wenye umbilikimo. Budalah alikuwa na uhusiano wa siri na msichana mwenye urefu wa wastani, na huyo rafiki yake akapata ujauzito. Mama wa binti alipotambua kuwa Budalah ndiye baba wa mtoto wa mwanaye alimnyonga mtoto na kumwozesha binti yake kwa mwanaume mwingine mrefu wa wastani. Hali kama hiyo ilijitokeza pia kwa Kaggwa baada ya dada zake wawili kufa, shangazi yake akamwambia: “Natamani ungekufa wewe Kaggwa kwa sababu hauna manufaa yoyote zaidi ya kuleta aibu katika familia, lakini badala yake Mungu kachukua watoto wa kawaida na wenye manufaa katika familia.”

Kama ilivyo kwa walemavu wengine, watu wenye umbilikimo wanakabiliwa na shida ya kupata huduma za afya. Kitabibu, kuna matatizo mengi yanayohusiana na umbilikimo wa aina fulani, kwa mfano, kuna hali kama achondroplasia, ambayo ni aina ya kawaida ya umbririkimo, dalili nyinigine ni pamoja na ugonjwa wa kutopumua usingizini, maambukizi ya sikio na matatizo ya kusikia, ugonjwa wa kichwa kikubwa, kupata kibyongo kwa watoto, ugonjwa wa kubana uti wa mgongo, maumivu ya mgongo, kupoteza uwezo wa kushika n.k. Matatizo haya yanahitaji huduma maalumu, ambazo ni adimu sana, na sehemu nyingine hazipo kabisa. Pamoja hayo, huduma

za kitiba zinazopatikana bado haziwafikii mbilikimo. Kina mama wanaokaribia kujifungua hukosa huduma za afya ya uzazi kabla ya kujifungua. Kuwepo kwa vitanda vinavyoweza kuongezwa au kupunguzwa urefu, au ngazi za kupandia vinaweza kuwasaidia mbilikimo kupata huduma kwa urahisi. Kuhamasisha mafunzo maalumu na kufanywa kwa utafiti kunaweza kusaidia kuboreshwa kwa huduma za afya kwa mambilikimo. Kwa kawaida, watu wenye umbilikimo wanahitaji huduma za afya sawa na watu wa kawaida.

Kiuhalisia, umbilikimo ni ulemavu tu kutokana na jamii yenyewe inavyoichukulia hali hii. Mambilikimo wanaweza kuishi maisha kamili na yenye thamani na wanaweza kutoa mchango mkubwa katika jamii, lakini wanahitaji mazingira jumuiishi na kujipanga kijamii kwa wao kuweza kufanya hayo.

Annet Nakyeyune ni Mkurugenzi na Mwanzilishi wa Shirika la “Little People of Uganda”.

“

Pia mbilikimo wanakabiliwa na hatari ya kuuawa wangali bado wadogo, kwa sababu sio jambo geni kwa familia nyingi kuwauwa watoto wanaozaliwa mbilikimo

”

JITIHADA ZA KUTAFUTA URAIA

Ninatokea Bahar al-Ghazal...Tuko watu saba nyumbani kwetu. Maisha yangu ni mabaya kwa sababu sina pesa wa wala kazi ya kufanya. Nahisi nimepotea. Watu ninaishi nao wana hofu na wasiwasi. Hadi sasa hawajui nini cha kufanya kwa sababu hakuna muafaka uliofikiwa na serikali. Wana hofu kubwa kwa sababu kuna matatizo mengi yatawakumba Sudani Kusini. Tungependa Serikali ya Sudani na Serikali ya Sudani Kusini kueleza mustakabali wetu na kama tuende au hapana. Sijioni salama. Nafikiri kwamba tunaweza tusiwe salama hata kama tutakwenda au tutabaki kwa sababu kuna matatizo mengi sana Sudani Kusini na watu wa hapa [Sudani Kaskazini] wanaweza wasikubali matokeo ya kutengana.

- Msudani Kusini anayeishi katika kambi ya Mandela mjini Khartoum

Mwezi Januari 2011 maelfu ya watu wa Sudani Kusini walipiga kura ya kutengana ili kuwe na taifa huru la Sudan Kusini. Tarehe 9 Julai, 2011, Sudani ya Kusini iliyojitenga na Jamhuri ya Sudani likawa taifa kamili. Nini mustakabali wa kisheria wa watu karibu milioni 1.5 wa kusini ambao walikimbilia Sudani Kaskazini kufuatia mapigano ya wao kwa wao ya muda mrefu, pia Wasudani Kaskazini waliopo Sudani Kusini?

Ni vigezo gani vitatumika kubainisha uraia wa watu wa Jamhuri ya Sudani au wa taifa jipya la Sudani kusini?

Licha ya majadiliano yaliyochukua miezi kadhaa, Serikali ya Sudani na chama cha Wapigania Uhuru wa watu wa Sudani (SLM) hadi kufikia tarehe 9 Julai walishindwa kufikia makubaliano juu ya uraia wa Wasudani. Pande hizi mbili walishidwa kutoa tamko lolote kwa wale waliathiriwa juu ya uhalali wa kisheria wa uraia na maisha yao ya baadaye ili waweze kufuata maelekezo. Hadi kufikia tarehe 9 Julai, Wasudani Kusini wote waliokuwa wanaishi Kaskazini ambao tayari walikuwa wanarudi Kusini, mara nyingi wamekutana na hali ngumu katika safari yao. Hadi mwanzoni mwa mwezi Mei mwaka huu, mashirika ya misaada wanaamini karibu Wasudani Kusini 300,000 walikuwa tayari wamerudi Sudani Kusini hadi kufikia kiangazi mwaka 2010. Walikadiria kwamba mwaka 2011 Wasudani wengi zaidi yapata watu 800,000 watarudi Sudani Kusini. Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR), wengi waliokuwa wanarudi Sudani Kusini kwa majira yale walidai walifanya vile kwa kuhofia uraia wao kama wataendele kuishi Kaskazini. Wakimbizi hao mara nyingi walirejea maneno ya Waziri wa Habari wa Serikali ya Sudani, Kamal Obeid, aliye tamka kupitia redio ya taifa mwaka jana, "Wao [Wakusini]

SUDANI

NA
JOANNA OYEDIRAN



**Kutengana huku
ni kutengana
kijiografia
au kutengwa
kiubinadamu?**

*- Mwanaume Msudan Kusini
anayeishi kambi ya Manderu,
Khartoum, Sudan Kaskazini
living in Mandela camp*

hawatafurahia haki za raia, kazi au manufaa, hawataruhusiwa kuuza wala kununua katika soko la Khartoum na hawatatibiwa hospitali... Hatutawapa hata bomba la sindano hospitali." Ingawa kwa hakika baadhi ya viongozi wa serikali ya Sudani walionesha kwamba Wakusini watalindwa, lakini hofu kufuatia vitisho vya kauli ya waziri haijafutika mioyoni mwao.

Kila nchi ina haki ya kuamua juu ya sheria za uraia. Hata hivyo, serikali haina mamlaka ya mwisho ya kipekee (carte blanche) . Sheria za kimataifa za haki za binadamu, zinaitaka serikali kwanza ihakikishe kuwa sheria za uraia sio za ubaguzi, ikiwemo ubaguzi wa kikabila na kijinsia, pili, kufanya kila linalowezezana kuhakikisha watu hawakosi uraia. Ingawa inaweza kugusa hisia za Wasudani wengi kwamba uraia katika mataifa mawili ya Sudani Kaskazini na Sudani Kusini unapaswa utolewe kwa wale wanaodhaniwa kuwa na wana mahusiano wa kijadi kwa aidha Kusini au Kaskazini, ni baadhi tu ya serikali za kibaguzi za Afrika ndio zinatoa uraia kwa vigezo vya ukabila. Katika sheria za kimataifa uraia unatolewa na serikali ya taifa ambalo mtu huyo ni makazi yake ya kudumu.

Kwa kushindwa kufikia muafaka Julai 9, pande zote mbili wanajaribu kuchukua hatua za kuwa na uraia wa aina moja. Mnamo mwezi Juni 2011, Bunge la Sudani kusini lilipitisha Sheria ya Uraia. Sheria hiyo inasema, mtu atatambulika kuwa raia wa Sudani Kusini kwa kuzaliwa wakati sheria hii imeanza kutumika ikiwa, a) ana wazazi, mababu au wazazi wa mababu waliozaliwa Sudani Kusini upande wa mama au upande wa baba; au b) anatoka katika moja ya makabila ya wazawa wa Sudani Kusini (hayajatajwa); c) amekuwa akiishi Sudani Kusini tangu Sudani ipate uhuru au d) amekuwa raia mwema wa taifa la Sudani Kusini kwa makazi ya kudumu. Ni mafanikio makubwa kuona kwamba masharti haya hayabagui wanawake wala wanaume katika

kupata uraia. Japokuwa ukabila ni moja ya masharti ya kupata uraia, lakini sheria iko wazi katika kuonyesha ni nani raia kwa kuzaliwa, pia kwa sharti la makazi. Lakini kwa Sudani, hadi wakati wa kwenda kweda kwenye vyombo vya habari mambo yalikuwa hayaeleweki, lakini kwa miezi kadhaa iliyopita, kauli za viongozi wa serikali ya Sudani zimekuwa zikionyesha kwamba Sudani itawavua uraia wa Sudani watu wanaodhaniwa kuwa walikuwa raia wa Sudani Kusini, ingawa katiba ya Sudani inawataka Wasudani wote kushikilia umoja wa kitaifa. Hatua hiyo itakuwa ya ubaguzi na inatengeneza mwanya mkubwa kwa watu wanaoangukia katika kundi hili kukosa uraia pande zote mbili.

Mbali na sheria za kimataifa, ziko sababu nyingi za kuwa na tafsiri ya uraia inayowajumuisha watu wote wa Sudani na Sudani Kusini kuwa ni njia nzuri. Tafsiri ya serikali ya nani na kwa jinsi gani apatiwe uraia inaonesha dhamira ya serikali hiyo. Serikali inayotanguliza ukabila katika kumtambua raia inajiweka katika hatari ya ukabila kutangulizwa katika kupata madaraka na rasilimali.

Serikali inayojumuisha, ambapo watu wote wana utaifa bila kujali asili yao au ya mababu zao waliishi eneo gani, wanaweza kuwa raia, na ni rahisi kuzitumia fikra hizi za umoja kugawa rasilimali za nchi na madaraka kwa umoja na bila ubaguzi.

Joanna Oyediran ni Meneja Programu wa OSIEA.





Kupanua wigo wa kupata
taarifa



WANASHERIA WANAWAKE WA ZANZIBAR NI JESHI CHIPUKIZI NA EMMA DAY

Wakiwa wamebanana katika chumba kidogo cha ofisi ya Mwanasheria Mkuu wameketi wanawake wanne wanasheria wanaofanya kazi kama mawakili wa serikali, na wanasheria wa kujitolea katika muda wao wa ziada kwenye Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA). Hamisa, Fatma, Amsa, na Chai ni wanasheria wachanga. Ni wahitimu wa Chuo Kikuu Cha Zanzibar ambacho kilifungua milango na kuanza kuchukua wanafunzi wa sheria miaka kumi tu iliyopita. Kabla Chuo Kikuu hakijaanzishwa Tanzania Visiwani, kulikuwa na wanasheria watatu tu Zanzibar nzima, lakini sasa wapo wapatao sabini, na wanawake hawa wanadai mabadiliko Zanzibar.

Zaidi ya asilimia 90 ya Wazanzibar ni Waislamu, na mfumo wa sheria wa Zanzibar umegawanyika sehemu mbili, mahakama za kawaida na Mahakama ya Kadhi ya

Waislamu. Kwa kesi zinazohusu sheria za kifamilia, Wazanzibar wanapeleka mashauri yao katika Mahakama ya kadhi. Mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kisheria pale ambapo washitaki wa pande zote ni waislamu, na inashughulikia tu maswala ya mgogoro ya ndoa, malezi ya watoto, matatizo ya kukimu mume, mke au watoto, na mirathi. Rufaa za kutoka katika ofisi hizi, hupeleka katika Ofisi ya Rufaa ya Kadhi na kisha kwenda Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Wanawake wanaodai haki katika mahakama ya Kadhi, kama ilivyo katika vyombo vingine vya sheria hujikuta wanapata upinzani kwa sababu baadhi ya makadhi huitafsiri Koran kwa jinsi ambayo haitambui uwepo wa haki sawa za kisheria kwa wanawake. ZAFELA inawasaidia wanawake ambao hufika ofisini kwao kufichua hatua zinachukuliwa na kuhakikisha haki za wateja wao zinapatikana.

Fatma alikuwa na miaka 16 alipoolewa na mwanaume katili ambaye alimzidi kwa miaka 19. Akiwa na miaka 19 kwa sasa, Fatma alidai talaka mwaka jana. Alikataa kumpa talaka na akamyang'anya mtoto wao wa miaka miwili. Fatma alipeleka mashtaka yake katika mahakama ya Kadhi wa wilaya ambako alishinda kesi na kuweza kupewa talaka yake na kurudishiwa mwanae wa miaka miwili. Lakini mume wake alikata rufaa na kadhi wa mahakama ya rufaa aliwambia Fatma awezi kupewa talaka, ni lazima arudishe mahari iliyolipwa kwa baba yake kabla ya kupewa talaka, na lazima arudi katika mahakama ya kadhi wa wilaya ili kurudishiwa mwanae. Fatma anasema atarudisha mahari iwapo tu mume wake atakubaliana kutimiza wajibu wake wa kisheria wa kutunza mtoto. Hajamuona binti yake tangu mume wake amchukue zaidi ya mwaka mmoja uliopita. ZAFELA

inamsaidia Fatma kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu.

Kwa sababu Chuo Kikuu kimekuwepo Zanzibar kwa muongo mmoja tu, hakuna mahakimu wa mahakama za mwanzo katika mahakama za kawaida wala za Kadhi ambao wamepitia mafunzo maalumu ya uhakimu. Kiuhalisi makadhi wengi hawakwenda shule. Wameisoma Koran kwa kina, lakini hawana maarifa ya kutosha ya kanuni za sheria za kawaida.

Kwa amri, wanasheria hawatakiwi kufika katika mahakama za mwanzo iwe ya mfumo wowote wa kisheria, huenda ni kwa sababu wanajua zaidi kuliko hakimu au kadhi muhusika. Wanasheria wa ZAFELA lazima wafanye kazi yao pembeni kuwashauri wateja wao jinsi ya wao wenyewe kujieleza kikamilifu. Inawezekana kukodi mtu mwenye maarifa kidogo ya kisheria ili akusaidie badala ya mwanasheria. Mtu huyu anaweza kujua mambo muhimu ya kisheria lakini hawezi kujenga hoja ya kupingana na hakimu. Ni katika mahakama kuu tu ndipo wanasheria wanaruhusiwa kuwakilisha wateja wao wenyewe.

Hamisa anasema ni vigumu kutumia hukumu kutoka mahakama za mwanzo za kadhi kwa sababu hazina taarifa wala maelezo ya kutosha juu ya tatizo lilivyowasilishwa na kupembuliwa ili kutoa maamuzi. Mahakama za kadhi zinatakiwa kutumia taratibu za sheria za serikali katika kuendesha kesi zao, lakini hawafanyi hivyo kwa sababu ya kukosa mafunzo. Hii inakuwa changamoto kwa ZAFELA kuwakilisha wateja wao wakati hawarusiwi kuingia katika chumba cha mahakama kusikiliza mashitaka na jinsi kesi inaendeshwa na maamuzi ya mahakama, na wala hakuna taarifa za maandishi zinazotolewa. Kwa sasa ZAFELA inapitia upya Sharia ya Mahakama ya Kadhi na wanatarajia kutoa mapendekezo kwamba, kadhi anatakiwa awe na angalau shahada ya kwanza ya sheria, ikiwemo sheria za waislamu (Sharia). Sheria za sasa haziiwaruhusu wanawake kuwa wanasheria lakini Jamila ambaye ni Mratibu wa

ZAFELA, anasema hili ni suala la tafsiri ya Koran tu. Hakuna kipengele maalum katika Koran kinachowakataza wanawake kuwa makadhi, bali ni wanaume ndio walioamua kuitafsiri hivyo. Wako makadhi wengi wa kike katika nchi nyingi mbalimbali ikiwemo Palestina, Indonesia na Malaysia.

Katika mfumo wa kimahakama, kadhi lazima aangalie kwanza katika Koran alafu akikosa jibu ndipo itamlazimu aangalie katika Hadithi za mafundisho ya Mtume Mohammed. Ikiwa bado hatapata ufumbuzi

Jamila anaweka wazi kwamba dini na utamaduni zimekuwa zikipotoshwa katika tafsiri ya sheria za Kiislamu

itambidi aombe msaada kwa mwanazuoni wa Shia mbaye atamsaidia kufanya maamuzi ya Kiislamu. Kwa Zanzibar wanazuoni wote wa Shia pia ni wanaume, na wengi wao waliosoma elimu ya vizazi vya zamani sana. Mmoja kati ya wanasheria wa kike alisema kwamba sio kweli kwamba Koran inasema lazima uvae kilemba na kufunika kichwa chote; badala yake inasema lazima ufunike kifua na pia haisemi kwamba ni wanaume tu ndio wanaotakiwa kuwa makadhi; inasema wanaume lazima wawe 'viongozi'. Lakini pia wanaume wanasema kwamba Koran inasema wanawake hawapaswi kupaza sauti zao katika hadhara wala kuwahoji wanazuoni wa Shia (ambao

wote ni wanaume) hivyo mjadala unaishia hapo. Jamila anasisitiza kwamba kimsingi Uislamu ni dini yenye usawa, na kwamba maendeleo yanawezekana kwa wanawake bila kupunguza kipengele hata kimoja cha dini yao.

Mabadiliko ambayo yameletwa na ZAFELA ni dhahiri. Miaka minane iliyopita wakati jamila alikuwa Chuo Kikuu masuala ya jinsia hayakuwepo katika masomo yao ya sheria. Wanafunzi wa sheria sasa wanachukua kozi za usawa wa jinsia na pia wanasoma mfumo wa Kadhi na kuukosoa wakiwa madarasani. ZAFELA wameweza kujiimarisha wenyewe kama wadau wa masuala ya sheria za watoto na wanawake Zanzibar. Hadi sasa popote panapofanyika mabadiliko ya sheria inayogusa wanawake na watoto ZAFELA wanahusishwa na kuombwa ushauri na serikali na mashirika ya umma, na sauti zao zinakuwemo katika mjadala. Mwezi Aprili 2011 ZAFELA ilirusha hewani kipindi cha masaa mawili cha moja kwa moja katika luinga ya Zanzibar, wakiuambia umma juu ya utafiti wao juu ya mfumo wa Kadhi na kuhimiza watu wachangie maoni katika mjadala. Watu waliweza kupiga simu na kutoa maoni yao na kujadili suala hili. Jamila alisema kwamba, japokuwa ulikuwa mjadala chanya kwa jamii, lakini kuna baadhi ya watu walipiga simu na kuishutumu ZAFELA kwamba inapingana na Uislamu, wakisema kwamba wanawake hawapaswi kuwahoji wanaume ambao ni viongozi wao, na kwamba kufanya hivyo ni kuuhoji Uislamu wenyewe.

Midahalo ya umma ndiyo chanzo cha mabadiliko, na inaleta mabadiliko yenye tija pale wanawake wapoongoza mijadala juu ya suala hili. Wanasheria wa ZAFELA wanalo tumaini kwamba mfumo wa Kadhi, na pia jamii ya Wanzibar watazidi kuitikia zaidi katika kuwapatia wanawake haki zao zote katika kipindi cha miaka michache ijayo.

Emma Day ni Mwanasheria wa kujitegemea huko Nairobi, Kenya.

044 | SAUTIZETU

HAKI ZA WAFUGAJI

NCHINI TANZANIA na Emma Day

MAENEO YA MALISHO YA WAFUGAJI YANAENDELEA KUONEKANA KUWA NI RASILIMALI YA UMMA YENYE FAIDA KUBWA AMBAYO INAWEZA KUTUMIKA KWA UTALII NA KULETA MAPATO KUTOKANA NA UWEKEZAJI WA NJE. DHANA YA UMILIKI WA ARDHI YA UMMA/ JUMUIYA IMEKUWA KWENYE VITISHO TANGU KUENZISHWA KWA SERA ZA UMILIKI WA ARDHI



Nchini Tanzania, kuna wafugaji takriban milioni 1.5 waliotawanyika kwenye makundi makuu matano ya jamii za wafugaji, Wamasai wakiwa ndio kundi kubwa na linalojulikana zaidi. Wafugaji siku zote wamekuwa wakisafiri pamoja na mifugo yao, wakitumia maeneo ya malisho ya mifugo yao tofautitofauti kutegemea na msimu, ambao huwahakikishia mifugo yao inapata mabwawa ya maji ya msimu, na pia kuacha ardhi ichipue nyasi tena kati ya kipindi na kipindi cha malisho. Kama mifugo itazuiliwa sehemu moja inakuwa na hatari ya kukumbana na ukame na magonjwa ya mifugo.

Dhana ya umiliki wa ardhi ya jumuiya imekuwa kwenye vitisho tangu kuanzishwa kwa sera za umiliki wa ardhi iliyorithiwa tangu kipindi cha wakoloni. Sheria ya umiliki wa ardhi imendelea kuwa kwenye hati hati katika kuleta ufanisi wa kulinda ya maisha

ya wafugaji. Matokeo yake ni kuwepo kwa utata wa sheria za ardhi katika nchi nyingi za Afrika Mashariki ambazo mara nyingi hazitekelezi kwa vitendo au hupuuzwa.

Kutokana na ongezeko la watu, mahitaji makubwa ya ardhi, uwekezaji wa kigeni, na sheria za ardhi ambazo hazilindi miliki za ardhi ya jumuiya, wafugaji wamejikuta maisha yao yako kwenye mashambulizi toka kwa serikali na kwa wananchi nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa muda mrefu, Sera za serikali za Afrika Mashariki zimesahau au hata kuidharau mifumo ya maisha ya wafugaji. Hii ilisukumwa kwa sehemu mawazo ya viongozi kufuata nadharia potofu ya muda mrefu ya kiikolojia inayodai kuwa mfumo wa maisha ya wafugaji unaharibu mazingira, na hivyo kutaka wafugaji wakae mahali pamoja eti kwa sababu ya kuhifadhi mazingira.

Nchini Tanzania, asilimia 28 ya ardhi imehifadhiwa kwenye makundi ya matumizi tofauti tofauti, sehemu kubwa ya ardhi hii

kiasili ni maeneo ya wafugaji. Sehemu kubwa ya ardhi iliyohifadhiwa na kulindwa na sheria ni Hifadhi za Taifa, na hifadhi kumi za taifa kati ya hifadhi kumi na nne za Tanzania zilianzishwa wakati wa wakoloni kiasili yakiwa maeneo ya wafugaji.

Hata hivyo, maeneo ya malisho ya wafugaji yanaendelea kuonekana kuwa ni rasilimali ya umma zenye faida kubwa ambayo inaweza kutumika kwa utalii na kuleta mapato kwa uwekezaji wa nje. Kwa serikali inapata fedha nyingi sana kwa kuwaondoa wafugaji kutoka kwenye maeneo yao ili ardhi ibadilishwe matumizi na kuwa hifadhi ya taifa kwa ajili ya watalii, au itengwe kwa ajili ya wawekezaji binafsi wanaolipa fedha serikalini. Cha kushangaza, Tanzania inawategemea kwa kiwango kikubwa wafugaji na wakulima-wafugaji kupata maziwa na nyama. Na mchango wa wafugaji kwenye uchumi wa taifa haulingani na mchango wa uwekezaji, wafugaji pekee wanachangia pato la taifa kwa asilimia 40.



Mwaka 1992, serikali ya Tanzania ilitenga eneo la Loliondo kwa kampuni ya uwindaji linaloendeshwa na kampuni ya Ortello Business Corporation.

Bila kujali maisha ya wafugaji ambao wameishi katika eneo hilo kwa miaka mingi, jamii za wafugaji katika eneo la hili waliondolewa kwa nguvu na kufanyiwa vitendo vya kigaidi na mamlaka zilizosimamia zoezi. Nyumba na makazi ya wafugaji zilichomwa moto na mifugo ya wafugaji iliondolewa kwa nguvu na kupeleka sehemu kavu kusiko na maji wala malisho mazuri, hali iliyopeleka mifugo mingi kufa. Baada ya kipindi kifupi, baadhi ya wafugaji wa Loliondo wameanza kurudi taratibu kwenye maeneo yao, na kuanza kujenga nyumba na maisha yao. Hatma ya baadaye ya maisha yao haijulikani.

Shirika lisilo la kiserikali la wafugaji asili (PINGOS), mwanachana wa jukwaa la mashirika yasiyo ya kiserikali takriban arobaini ya wafugaji, wawindaji na waokota matunda. Shirika hili linalenga kuweka wazi na taarifa za ukiukaji wa haki za binadamu unaofanywa dhidi ya jamii za wafugaji. Shirika la PINGOS hufanyakazi kwa karibu sana na shirika lisilo la kiserikali Taasisi ya utafiti wa Haki za Ardhi na Rasilimali (Haki Ardhi), lililoko Dar es Salaam. Mashirika haya mawili hivi karibuni kwa kushirikiana na Kituo cha Sheria na Haki za Bindamu (LHRC), Mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali Ngorongorona Asasi ya Ujamaa yamefungua kesi ya kikatiba Mahakama Kuu ya Tanzania kuitaka mahakama izuiye serikali na kampuni ya Ortello Business Corporation kukoma kuwaondoa wafugaji na kukiuka haki za binadamu eneo la Loliondo. Lengo la kesi haya mahakamani ni kuamiriwa kwamba ardhi ya Loliondo ni ya wafugaji wa eneo hilo. Hadi kipindi kilipoandikwa makala haya, uamuzi ulikuwa bado haujulikani maana Mahakama ya Tanzania haina historia ya kutetea wafugaji. Uwekezaji binafsi nchini Tanzania unachukuliwa kama ni kwa maslahi ya umma, kwa hiyo

ardhi bila kujali ni ya mfugaji au mkulima mdogo inaweza kuchukuliwa kwa misingi ya uwekezaji binafsi, na Majaji kwa ujumla hawachagui kuifafanua sheria kwa msingi wa kuwapatia haki wafugaji.

Kufukuzwa wafugaji katika eneo la Loliondo ni sehemu tu ya orodha ya kuondolewa kwa wafugaji toka ardhi yao ya asili kulikofanyika ndani ya miaka michache tangu Rais Kikwete aingie madarakani. Kupitia mfumo wa “ardhi ya hifadhi” uliotangazwa sana nchini, eneo kubwa la ardhi ya wafugaji limechukuliwa kwa njia hii ili kubadilishwa kuwa hifadhi ya asili kwa ajili ya watalii, au kuwatengea wawekezaji binafsi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kati ya mwezi Oktoba mwaka 2006 na mwezi Mei mwaka 2007 serikali ya Tanzania iliwaondoa kwa nguvu wafugaji kwenye eneo la Mbarali mkoa wa Mbeya baada ya serikali kulitangaza eneo hilo kuwa ni eneo la hifadhi. Wakati wa zoezi la kuwaondoa wafugaji hao kwa nguvu, watu walipigwa hovy, familia zilitenganishwa, huku watoto, akina mama na wazee wakiachwa bila ulinzi wala chakula. Wafugaji wengi waliibiwa au kunyang'anywa mifugo yao, na walitozwa faini kubwa ya uharibifu wa mazingira. Mamlaka za wilaya zilianza kukamata ng'ombe za wafugaji na kuzizuia sehemu moja na kuwatoza faini kali wafugaji ili mifugo yao iachiwe huru. Mamlaka za serikali ya wilaya ya mbarali waliweka mfumo ambao uliwalazimisha wafugaji kuuza mifugo yao kwa bei ya chini sana ya viwango vya soko. Maafisa wa serikali wala rushwa wakatamia fursa hiyo ya bei ya kutupwa kununua mifugo kwa bei karibu na bure, na kudai hongo kwa wafugaji katika kila kizuizi kilichowekwa kwenye maeneo ya kupitishia mifugo hiyo. Wafugaji walipinga suala hili kwa kufungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania, kesi ambayo hadi leo bado haijaamuriwa.

Kwa mujibu wa shirika la PINGOS, wakala wa serikali wa hifadhi za taifa “Mamlaka

za Hifadhi za Taifa Tanzania” (TANAPA), iliripoti kuwa imetenga kiasi cha dola za Kimarekani milioni kadhaa kwa ajili ya kuwalipa fidia waathirika wa kuondolewa wafugaji huko mbarali. Hata hivyo, fedha hizi zilililiwa na watendaji wala rushwa na hazikuwa faidisha chochote wafugaji walioathirika na hamahama. Shirika hili linaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) kuchuka hatua za makusudi kuchunguza tuhuma za vitendo vya rushwa kwenye utekelezaji wa zoezi la kuwahamisha wafugaji wilayani Mbarali.

Asasi za Haki Ardhi na PINGOS zimepanga kutekeleza mradi wa kuzijengea uwezo jamii za wafugaji kutunza kumbukumbu, kutoa taarifa na kukabiliana na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu wanavyokumbana navyo. Wafugaji toka jamii mbalimbali watashiriki katika mdahalo huo ambao watapatiwa taarifa kuhusu haki za binadamu na sheria. Inatarajiwa kuwa mradi huu utaziwezesha jamii za wafugaji kufahamu na kupata ujuzi wa kujipanga na kuhamasishana wenyewe kudai haki zao kupitia wawakilishi wa serikali za mitaa. Pia Haki Ardhi na PINGOS zimepanga kuishawishi serikali kuboresha sheria na sera zilizopo abazo kwa sasa zinazuia na kuwanyima wafugaji haki ya kuwa na ardhi. Kwa mujibu wa Haki Ardhi, mbinu ya kujengea uwezo jamii ni muhimu sana kwa sasa, maana mabadiliko ya suala fulani huletwa na watu walioathirika na suala hilo.

Mashirika haya yanaona mjadala wa wananchi unaoendelea kuhusu Katiba mpya ya Tanzania ni fursa ya kipekee. Inatarajiwa kuwa kupitia mchakato jumuishi wa kupitia upaya katiba, wabunge wataweza kuandaa rasmiu ya katiba mpya itakayokuwa na vipengele vya kisheria juu ya haki ya ardhi ambavyo vitalinda waziwazi haki za jamii za wafugaji.

Emma Day ni Mwanasheria wa Kujitegemea aliyeko Nairobi, Kenya.

Kutokomeza ubaguzi na
unyanyapaa wa kijamii
makundi yaliyotengwa

NA EMMA DAY

WANANCHI DARAJA LA PILI : WANUBI

Zam Obed ameishi maisha yake yote eneo la Kibera, eneo kubwa zaidi la makazi yasiyo rasmi mjini Nairobi. Akiwa Mnubi, ni mzaliwa wa ukoo wa jamii ya Kiislamu kutoka Milima Nuba Sudani kusini, watu walioletwa nchini Kenya na Waingereza ili wahudumu kwenye jeshi la kikoloni la Waingereza. Kufuatiwa kutawanyika kwao, waingereza hawakuweka sheria yeyote ya kuwarudisha wanubi Sudani, au kurasmisha haki zao kupata ardhi nchini Kenya. Badala yake, Wanubi walitengewa ardhi hekari 4,197 eneo la Kibera mjini Nairobi, ambako waliruhusiwa kuishi, lakini bila kuwa na haki rasmi ya uraia. Eneo hilo ndipo Wanubi zaidi ya 100,000 wanaishi hadi leo, na ardhi yao imepunguzwa hadi kuwa chini ya hekari 400 sehemu kubwa ikiwa ni eneo la makazi duni. Serikali haitambui haki ya Wanubi ya ardhi ya babu zao eneo la Kibera, inawaona kama wakazi wavamizi kwenye ardhi ya serikali.

Zam anasema kwamba masuala ya ardhi yanayowasumbua Wanubi nchini Kenya yanatokana na suala la utambulisho wa asili yao. Chini ya Sheria ya Usajili wa Watu kila raia wa Kenya ni lazima aombe Kitambulisho cha taifa pindi anapofikisha umri wa miaka 18, au vinginevyo anakabiliwa na adhabu ya kosa la jinai. Kwa Wakenya wengi huu ni mchakato mwepesi usio na shida yeyote, lakini kwa Wanubi lazima kwenda mbele ya Kamati ya Uchunguzi yenye Viongozi wa Jadi, Afisa Tarafa, Kikosi cha Usalama wa Taifa na Ujasusi, Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, na jopo la wazee wa jadi, ambao huamua kama wakubali ombi lako au la.

Wanubi wengi kwa mujibu wa Katiba wana haki ya uraia wa Kenya, kwa sababu kama alivyo Zam, wengi wao wamezaliwa nchini Kenya kama walivyokuwa wazazi na babu zao ambao pia walizaliwa Kenya. Mawazo kwamba Wanubi si raia wa Kenya hayana msingi na ni fikra za kibaguzi. Kulingana na utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Shirika la Open Society Initiative (OSJI), asilimia 37 ya Wanubi nchini Kenya hawana nyaraka za kumbukumbu zozote za kisheria kuhusu uraia wao na wengine walipata nyaraka hizo baada ya jitihada kubwa. Zam alipata bahati tu kwani baba yake alikuwa na mtu anayemfahamu katika Ofisi ya Wilaya, hivyo hakupitia mchakato wa kuchunguzwa na akapata kitambulisho chake kiurahisi na haraka.

Mbali na umuhimu wa kitambulisho cha taifa kuwa kama kiashiria cha uraia, vikwazo wanavyokutana navyo Wanubi katika kupata nyaraka hizi muhimu, vinawazuia kushiriki kikamilifu kwenye masuala ya kijamii kama Wakenya. Kitambulisho cha Taifa ni hati muhimu kwenye nyanja zote za haki za ambazo Wakenya wengine huzipata na kufurahia ikiwemo haki ya ajira, elimu, haki ya kupiga kura, kufungua akaunti benki, kusafiri, kununua vitu na kufanya kazi kama askari polisi au askari jeshi. Pia kinaweka ulinzi dhidi ya manyanyaso ya polisi na kukamatwa kiholela. Kwa kifupi, kitambulisho cha taifa ni sawa na uraia wenyewe, na bila kuwa nacho Wanubi wanafanywa kuwa hawana taifa, kitu ambacho ni kinyume na sheria za kimataifa.



Licha ya mahusiano ya baba yake na maafisa katika Ofisi ya Wilaya, Zam hakuwa na bahati tena alipooomba hati ya kusafiria (pasipoti). Mwaka 1997, katika kutambua mafanikio yake kitaaluma, Zam alipewa tuzo muhimu maishani mwake; udhamini kwenda kusoma ng'ambo katika chuo kikuu kimoja nchini Marekani. Akiwa na furaha na matumaini ya kufanikiwa maisha yake ya baadaye, Zam bila kuchelewa alituma maombi ya kupata hati ya kusafiria (pasipoti), lakini baada ya kusubiri kwa miezi kadhaa alipata barua ikisema kuwa hakuwa na sifa ya kuwa Mkenya, na hakuna sababu zilizotolewa. Baadaye Zam alipokea barua nyingine ikimtaka apeleke ushahidi wa uraia wake kwa kuonesha cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha taifa, na vyeti viwili vya kumaliza shule. Zam alipeleka vielelezo na taarifa zote zilizotakiwa na baada ya mwezi mwingine kupita aliamua kufuatilia kwa sababu alikuwa na wasiwasi wa kuchelewa kukamilisha mahitaji ya udhamini kutakakomfanya akose fursa hiyo. Zam aliambiwa kuwa faili lake limepotea kwa bahati mbaya na hivyo anapaswa kuomba upya. Kwa kuvunjika moyo, Zam alikata tamaa kufuatilia ombi la pasipoti.

Mwaka 1999, rafiki yake Zam alimshauri aende kubisha hodi kwa Afisa Mwandamizi wa Uhamiaji. Rafiki yake alikuwa wa kabila moja na Afisa wa Uhamiaji, na alikuwa tayari kumsindikiza ofisini kwa Afisa huyo. Afisa wa uhamiaji alishangazwa na ujasiri wa Zam kwenda ofisini mwake. Afisa huyo alipiga simu moja tu, na ndani ya dakika saba faili la Zam, ambalo alikuwa ameambiwa kuwa limepotea, kimiujiza lililetwa mezani kwake, na akamwelekeza Zam kwenda kwa naibu wake akasaidiwe. Naibu akampeleka Zam kwa Afisa anayeshughuka na masuala ya 'Waislamu na Wageni', ambaye naye alimpa Zam orodha ndefu ya kuleta nyaraka 17. Kwa kiwango fulani Zam aliweza kukusanya

nyaraka alizoambiwa na akarudi siku ya pili, na kumshangaza afisa Afisa huyo. Naibu Afisa hakuwa na kisingizio tena ikabidi atoe pasipoti kwa Zam tarehe 30 Julai 1999. Mafanikio haya kwa Zam yalikuwa ni matamu na kwa upande mwingine machungu, maana alipata kitu alichokitamani (pasipoti), ambacho kwa mujibu wa shirika la OSJI ni asilimia 2 tu ya Wanubi ndiyo wana pasipoti, hata hivyo, tayari muda wa udhamini kwa masomo yake nje ya nchi ulikuwa umepita tangu Julai 20, 1999.

Ukizungumza na Zam mara moja utapata hisia ya uhodari wa tabia yake. Kwa sasa ana umri wa miaka 39 na mama wa watoto wawili, Zam hajawahi kutoka nje ya Kenya, ukizingatia kuwa alipoteza fursa ya kusoma na kusafiri nje ya nchi aliyopata wakati wa ujana wake. Matumaini ya Zam kwa sasa yamegemea zaidi kwenye mustakabali wa maisha ya watoto wake, na kuna dalili kuwa mambo yanabadilika nchini Kenya kwa Wanubi wa kizazi cha sasa walicho watoto wake. Uamuzi wa kihistoria ulitolewa tarehe 25 Machi 2011, ambapo Kamati ya wataalam wa Kiafrika juu ya Haki na Ustawi wa watoto toka makundi ya *Wanubi wachache nchini Kenya*, ilisema wazi kuwa Kenya ni inavunja haki za watoto jamii ya Wanubi kwa kuwanyima utaifa, kubaguliwa na kushindwa kuwalinda dhidi ya kukosa uraia wa taifa. Kesi hiyo ilifunguliwa na watoto Wakinubi kupitia Washauri wao ambao ni shirika la OSJI na Taasisi ya Haki za Binadamu na Maendeleo ya Afrika (IHRDA). Hii ni mara ya kwanza kwa Kamati ya kufungua kesi dhidi ya serikali kuhusiana na haki za watoto, hatua ambayo inaonesha mafanikio makubwa zaidi kwa jamii Wanubi.

Mwezi Januari 2011 Shirika la Kiislamu linalotetea Haki za Binadamu (MUHURI) , kwa ufadhili wa shirika la OSIEA waliandaa

hati ya malalamiko wakiwa na El-Busaidy Abdulhaleem, dhidi ya uongozi wa serikali za mitaa mjini Mombasa, kupinga waraka wa wa kibaguzi wa serikali uliokuwa unaagiza kuwa Waislamu, Waarabu na Waasia lazima wapeleke vyeti vya kuzaliwa vya babu zao na vyeti vya kidini ili wapatiwe vitambulisho vya taifa. El-Busaidy alinyimwa Kitambulisho cha taifa mwaka 2010 kwa sababu hakuweza kupeleka vyeti vya kuzaliwa vya babu yake kama waraka ulivyotaka. Hatua ya kwanza ya kesi ilifanikiwa na mwezi Januari 2011 amri ya zuio ilitolewa na Mahakama Kuu ya Kenya mjini Mombasa, kuizuia Ofisi ya Taifa ya Usajili kutumia vipengele vya kibaguzi vya waraka, na amri hii ilitibitishwa na mahakama mwezi februari 2011 kwa misingi kwamba ubaguzi huo wa kabila na dini unavunja Katiba mpya ya Kenya ya mwaka 2010.

Usikilizaji kamili wa kesi ya Mombasa unaweza kuahirishwa kwa sasa kusubiri matokeo ya ripoti ya Kikundi Kazi juu cha masuala ya Uraia. Kikundi Kazi kimepewa jukumu la kuja na sheria mpya ya uraia ambayo itaendana na matakwa na vipengele vya ya Katiba mpya , ambapo pamoja na mambo mengine itashughulikia suala la baadhi ya wananchi kutokuwa raia wa taifa lolote. Madai haya ni sehemu tu ya kazi ya utetezi inayoendelea kukishawishi Kikundi Kazi kushughulikia ubaguzi unaowakabili Wanubi kama Zam nchini Kenya.

Emma Day ni Mwanasheria wa Kujitegemea aliyeko Nairobi, Kenya.



Wananchi makini na
na wenye
ufahamu





OSIEA THE OPEN SOCIETY INITIATIVE
 **FOR EASTERN AFRICA**



7 8 - 0 - 9 8 3 8 6 4 7 - 0 - 7